JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA KIDATO CHA NNE (CSEE) 2022

## ELIMU YA DINI YA KIISLAMU

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA KIDATO CHA NNE (CSEE) 2022

# 015 ELIMU YA DINI YA KIISLAMU

Kimechapishwa na:
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es salaam, Tanzania

**© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2023**

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO


DIBAJI....................................................................................................iv

1.0 UTANGULIZI.............................................................................................1

2.0 TATHMINI YA KILA SWALI...........................................................................3

2.1 SEHEMU A: Majibu ya Kuchagua na Kuoanisha.......................................3
2.1.1 Swali la 1: Kuchagua Jibu Sahihi.......................................................3
2.1.2 Swali la 2: Nguzo za Uislamu.............................................................13
2.2 SEHEMU B: Majibu Mafupi...............................................................16
2.2.1 Swali la 3: Qur'an.........................................................................16
2.2.2 Swali la 4: Nguzo za Imani...............................................................20
2.2.3 Swali la 5: Familia ya Kiislamu..........................................................23
2.2.4 Swali la 6: Historia ya Uislamu Baada ya Kutawafu Mtume (S.A.W) 26
2.2.5 Swali la 7: Nguzo za Uislamu.............................................................29
2.2.6 Swali la 8: Mfumo wa Jamii ya Kiislamu..............................................32
2.2.7 Swali la 9: Haki na Uadilifu katika Uislamu.........................................37
2.3 SEHEMU C: Maswali ya Insha...............................................................40
2.3.1 Swali la 10: Nguzo za Uislamu...........................................................41
2.3.2 Swali la 11: Sunnah na Hadith...........................................................47
2.3.3 Swali la 12: Qur'an........................................................................51
2.3.4 Swali la 13: Dola ya Kiislamu Madina................................................55

3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU KWA KILA MADA.................................................61

4.0 HITIMISHO.............................................................................................62

5.0 MAPENDEKEZO.......................................................................................63

Kiambatisho Cha Pekee.................................................................................64


## DIBAJI

Taarifa hii ya Uchambuzi wa Majibu ya Watahiniwa katika Mtihani wa Kidato cha Nne (CSEE) 2022 katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu imeandaliwa ili kutoa mrejesho kwa watahiniwa, walimu, wazazi, watunga sera na wadau wa elimu kwa ujumla kuhusu ufaulu wa watahiniwa katika somo hili. Katika taarifa hii uchambuzi umefanyika katika majibu ya watahiniwa kwa kuwa mtihani ni kiashiria kimojawapo kinachoonesha mambo ambayo watahiniwa hao waliweza kujifunza kwa usahihi na yale ambayo hawakuweza kujifunza katika kipindi cha miaka minne ya Elimu ya Sekondari.

Taarifa hii imeweka bayana jinsi ambavyo watahiniwa wameweza kupata alama za juu, wastani na za chini katika kila swali. Aidha, sampuli za majibu ya watahiniwa waliofanya vizuri na wale waliofanya vibaya zimeoneshwa. Vile vile, sababu mbalimbali zilizochangia baadhi ya watahiniwa kuweza kujibu maswali kwa usahihi zimeelezwa. Miongoni mwa sababu hizo ni pamoja na; kuelewa vema matakwa ya maswali na kuwa na maarifa ya kutosha juu ya mada mbalimbali za somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu. Aidha, uchambuzi umebaini kuwa watahiniwa walioshindwa kujibu maswali kwa usahihi walikosa maarifa katika baadhi ya mada za somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu na wengine walishindwa kubaini matakwa ya maswali. Uchambuzi umebaini pia udhaifu katika kujenga hoja katika kujibu maswali ya kujieleza kwa ufupi na yale ya insha.

Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa mrejesho uliotolewa utawawezesha wadau wa elimu kuchukua hatua madhubuti za kuboresha mchakato wa ufundishaji, ujifunzaji na upimaji ili hatimaye kuondoa changamoto zilizoainishwa katika taarifa hii na hatimae kuongeza kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika kipindi kijacho.

Baraza la Mitihani la Tanzania linatoa shukrani na pongezi za dhati kwa wote waliohusika katika kuandaa taarifa hii ya uchambuzi.



Dkt. Said A. Mohamed
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii ni matokeo ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa waliofanya Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne (CSEE) mwezi Novemba mwaka 2022 katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu. Mtihani huu uliandaliwa kwa kuzingatia muhtasari wa somo husika uliotolewa mwaka 2012 kwa Kidato cha I hadi IV.

Maswali yaliyotumika katika Mtihani yaliandaliwa kutoka katika mada kumi na nane (18) kati ya ishirini (20) zilizopo katika muhtasari wa somo. Aidha, maswali hayo yaligawanywa katika sehemu tatu; A, B na C zenye jumla ya alama 100. Sehemu A ilikuwa na maswali mawili (1 na 2), sehemu B ilikuwa na maswali saba (3 hadi 9) na sehemu C ilikuwa na maswali manne (10 hadi13). Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote katika sehemu A na B kisha kuchagua maswali matatu kati ya manne kutoka sehemu C.

Watahiniwa waliosajiliwa kufanya Mtihani wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu mwaka 2022 walikuwa 87,007 kati yao watahiniwa 84,230 sawa na asilimia 96.81 walifanya mtihani. Idadi hii inaonesha ongezeko la wanafunzi 8,093 ikilinganishwa na wanafunzi 76,137 waliofanya mtihani wa somo hili mwaka 2021. Kati ya watahiniwa 84,230 waliofanya mtihani mwaka 2022, watahiniwa 41,030 walifaulu katika madaraja mbalimbali. Jedwali lifuatalo linaonesha madaraja ya watahiniwa hao ikilinganishwa na mwaka 2021.

Jedwali Na. 1: Ulinganifu wa Ufaulu kati ya Mwaka 2021 na 2022

| MWAKA | % YA UFAULU | MADARAJA | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | A | B | C | D | F |
| 2021 | 47.09 | 03 | 169 | 8,322 | 27,177 | 40,074 |
| 2022 | 49.06 | 41 | 506 | 11,641 | 28,842 | 42,597 |

Jedwali Na. 1 linaonesha kuwa kiwango cha ufaulu kwa mwaka 2022 ni asilimia 49.06 ikilinganishwa na mwaka 2021 ambapo ufaulu ulikuwa asilimia 47.09. hali hiyo inaashiria kuongezeka kwa kiwango cha ufaulu kwa mwaka 2022 kwa asilimia 1.97 ikilinganishwa na mwaka 2021.

Aidha, kupanda kwa ufaulu huo kulichangiwa na kukua kwa uelewa kuhusu dhana ya upimaji wa umahiri kwa wadau na kuakisi kuwepo kwa mabadiliko chanya katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

Taarifa hii imechambua majibu ya watahiniwa katika kila swali kwa kulinganisha matakwa ya swali husika na majibu yake na kile ambacho watahiniwa wamejibu. Aidha, sampuli za majibu ya watahiniwa zimeambatanishwa ili kuonesha namna watahiniwa walivyojibu maswali mbalimbali. Taarifa hii imebainisha changamoto zilizowakabili watahiniwa katika kujibu maswali ili zifanyiwe kazi. Pamoja na uchambuzi wa majibu ya watahiniwa, taarifa hii imebainisha ufaulu wa watahiniwa hao katika mada mbalimbali zilizopimwa. Madaraja ya ufaulu katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu yalikuwa kama ifuatavyo:

Jedwali Na. 2: Madaraja ya Ufaulu Somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu

| ALAMA | DARAJA | MAONI |
|---|---|---|
| 75 - 100 | A | Vizuri Zaidi |
| 65 - 74 | B | Vizuri Sana |
| 45 - 64 | C | Vizuri |
| 30 - 44 | D | Inaridhisha |
| 0 - 29 | F | Dhaifu |

Jedwali Na. 2 linaonesha kuwa daraja la juu la ufaulu katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu ni A na daraja la mwisho ni F. Pamoja na kuwepo kwa madaraja hayo matano ya ufaulu, taarifa hii itatumia madaraja matatu katika kuwasilisha ngazi za ufaulu ambayo ni: vizuri, wastani na dhaifu. Ufaulu utakuwa dhaifu ikiwa asilimia ya watahiniwa waliofaulu katika swali ni 0 hadi 29. Ufaulu utakuwa wa wastani ikiwa watahiniwa waliofaulu katika swali ni kati ya asilimia 30 hadi 64 na ufaulu utakuwa mzuri ikiwa asilimia ya watahiniwa waliofaulu katika swali hilo ni 65 hadi 100.

Aidha, hitimisho na mapendekezo kutokana na uchambuzi wa majibu ya watahiniwa umetolewa katika sehemu ya mwisho ya taarifa hii. Inatarajiwa kuwa matokeo ya uchambuzi huu yatatumika katika kuimarisha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu kwa wanafunzi na hatimaye kuboresha kiwango cha ufaulu katika mitihani ijayo.

## 2.0 TATHMINI YA KILA SWALI

Tathmini ya kila swali imefanyika kwa kubainisha alichotakiwa kufanya mtahiniwa kwa mujibu wa matakwa ya swali, umahiri uliokusudiwa katika swali au kipengele husika, kisha idadi ya watahiniwa waliojibu swali hilo na kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika kila swali.

## 2.1 SEHEMU A: Majibu ya Kuchagua na Kuoanisha


Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili (1 na 2). Swali la kwanza lilikuwa la kuchagua jibu sahihi kutoka katika machaguo matano (A, B, C, D na E). Swali hilo lilikuwa na vipengele kumi na tano (15) ambapo kila kimoja kilikuwa na alama 1 hivyo swali zima lilikuwa na alama 15. Swali la pili lilikuwa la kuoanisha lenye vipengele vitano (5) ambapo kila kimoja kilikuwa na alama 1 hivyo, swali zima lilikuwa na alama 5. Kwa ujumla sehemu hii ilikuwa na alama 20.

### 2.1.1 Swali la 1: Kuchagua Jibu Sahihi

Swali la 1 lilikuwa na vipengele kumi na tano (i) - (xv) kutoka katika mada za: *Mtazamo wa Uislamu juu ya Elimu, Imani ya Kiislamu, Kumjua Mwenyezi Mungu (S.W), Mtazamo wa Uislamu juu ya Dini, Nguzo za Uislamu, Mtazamo wa Uislamu juu ya Ibada, Mambo ya Lazima Kufanyiwa Maiti Muislamu, Fiqh, Sunnah na Hadith, Qur'an, Dini sahihi anayostahiki mwanadamu, Historia katika Uislamu, na Bara Arab zama za Jahiliyah karne ya 6 A.D.* Mtahiniwa alitakiwa kuchagua jibu sahihi kati ya machaguo matano aliyopewa (A, B, C, D na E) kisha kuandika herufi ya jibu hilo katika kijitabu chake cha kujibia.

Takwimu zinaonesha kuwa swali hili lilijibiwa na watahiniwa wote 84,230 (100%) waliofanya mtihani. Kati yao watahiniwa 45,154 (42.61%) walipata alama 0 hadi 4 ambao ni ufaulu dhaifu. Watahiniwa

35,676 (42.36%) walipata alama 5 hadi 8 ambao ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 3,400 (4.04%) walipata alama 9 hadi 15 ambao ni ufaulu mzuri. Muhtasari wa ufaulu wa watahiniwa hao kwa asilimia ni kama unavyoonekana katika chati Na. 1.




**Chati Na. 1:** *Asilimia ya ufaulu wa watahiniwa katika swali la 1*

Chati Na. 1 inaonesha kuwa, ufaulu katika swali ulikuwa wa wastani kwani asilimia 46.39 ya watahiniwa walipata alama 5 hadi 15 ikilinganishwa na asilimia 53.61 waliopata alama hafifu.

Aidha, watahiniwa waliofaulu walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada nyingi zilizounda vipengele mbalimbali vya swali na waliweza kubaini matakwa ya vipengele hivyo. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika kila kipengele umefanyika kama ifuatavyo;

Katika kipengele cha (i) mtahiniwa alitakiwa kubainisha sifa ya Elimu yenye manufaa kwa mujibu wa Uislamu. Kipengele hiki kilipima uwelewa katika dhana ya elimu kwa namna ilivyobainishwa na Uslamu. Watahiniwa walioelewa vema dhana hiyo walichagua jibu sahihi C *Inawezesha kufanya Ibada*, jibu hili linabainisha uhusiano wa maarifa yote ya mwanadamu na kazi yake kuu hapa duniani. Kwa upande wa watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi, baadhi yao walichagua vipotoshi A *Inahusisha Dini na dunia* na B *Inafundisha ya Dunia na Akhera.* Vipotoshi hivo vilieleza dhana potofu juu ya mgawanyo wa elimu ambao kiasili makundi hayo hayawezi kutenganishwa. Wengine walichagua herufi E *Inatoa ujuzi na maarifa.* Watahiniwa hao

walishindwa kuelewa kuwa ujuzi na maarifa hauna manufaa yoyote kwa mwanadamu ikiwa haujamuwezesha kutekeleza wajibu wake ipasavyo.

Wengine walichagua kipotoshi D *Inasababisha kupata ajira,* Hoja ambayo haikuwa sahihi kwa sababu kupata ajira haitoshelezi kufasiri dhana ya elimu yenye manufaa kwa mujibu wa Uislamu. Kwa ujumla, Uislamu umeeleza dhana ya elimu yenye manufaa kuwa ni ile inayosababisha mtu kupata radhi za Mwenyezi Mungu (S.W) kwa kutimiza wajibu wake ipasavyo.

Kipengele cha (ii) mtahiniwa alitakiwa kubainisha kundi linaloonesha vigawe sahihi vya Tawhiid. Kipengele hiki kiliwapima watahiniwa umahiri wa kuchambua itikadi ya Kiislamu hususani katika upweke (umoja) wa Mwenyezi Mungu (S.W). Jibu sahihi katika kipengele hiki lilikuwa herufi D *Uluhiyyah, Rububiyyah na Asmaai wa swifat*, ambapo watahiniwa weledi katika dhana ya Tawhiid waliweza kuchagua jibu hilo.

Aidha, baadhi ya watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi walichagua kipotoshi C *Uluhiyyah, Asmaaiwaswifat na Ibadah,* ambalo halikuwa sahihi kwa sababu *Uluhiyyah* na *Ibadah* ni tanzu zenye maana moja. Wapo waliochagua B *Swifatiyya, Uluhiyyah na Rubbubiyyah*, ambalo nalo halikuwa sahihi kwa sababu hakuna tanzu kamili ya Tawhiid inayoitwa *Swifatiyya*. Kadhalika, waliochagua kipotoshi E *Rububiyyah, Asmaaiyyah na Swifaatiyya,* hawakuwa sahihi kwa kuwa katika kipotoshi hiki zilitajwa tanzu mbili tu za Tawhiid badala ya tatu. Wengine walichagua kipotoshi A *Uluhiyyah, Rububiyyah na Asmaaiyya.*Watahiniwa hao pia hawakuwa sahihi kwani katika tanzu za Tawhiid kamili hakuna inayoitwa *Asmaaiyya*. Watahiniwa hao kwa ujumla walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu Dhana ya Tawhiid na Tanzu zake.

Katika kipengele cha (iii) mtahiniwa alitakiwa kuonesha sababu ya Wahyi kuwa njia muhimu kwa watu kumjua Mwenyezi Mungu (S.W). Kipengele hiki kilikusudiwa kuwapima watahiniwa umahiri wa kutumia maarifa yao kubaini umuhimu wa *Wahy* katika kumtambua Mwenyezi Mungu (S.W). Watahiniwa walioelewa vema njia za kumjua Mwenyezi Mungu (S.W) walichagua jibu sahihi D *Ni njia inayofafanua wazi itikadi sahihi kwa watu*. Watahiniwa hao walielewa vema kwamba Wahyi ndio

njia kuu inayobainisha wasifu wa Mwenyezi Mungu kwa uhalisia wake na namna tunavyopaswa kumueleza na kumuelekea.

Aidha, watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki kwa ujumla hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu njia za kumjua Mwenyezi Mungu. Miongoni mwao walichagua kipotoshi E *Ni njia pekee iliyotumiwa na Mtume (S.A.W)* watahiniwa hao walishindwa kuelewa kuwa njia hiyo ilitumiwa na Mitume wote sio Muhammad (S.A.W) pekee. Wengine walichagua kipotoshi A *Ni njia pekee ya kumjua Mwenyezi-Mungu (S.W)* hoja ambayo haikuwa sahihi kwa sababu zipo njia kadhaa za kumjua Mwenyezi Mungu zilizotajwa katika Qur'an kama vile Fitrah, Historia na maisha ya Mitume, Nafsi ya mwanadamu na Mazingira. Wapo pia waliochagua kipotoshi C *Ni njia ya kwanza iliyopo moyoni mwa watu* hoja ambayo si sahihi kwani sifa ya iliyotajwa katika kipotoshi hiki inafahamika kama *Fitrah* sio *Wahyi*. Watahiniwa wengine walichagua kipotoshi B *Ni njia ambayo haiwezi kubadilishwa Kimaana,* hoja hii haikuwa sahihi kwa sababu wapo watu waovu ambao wanakusudia kuwapoteza wengine kwa kujaribu kubadilisha maana ya Wahyi.

Kipengele cha (iv) mtahiniwa alitakiwa kubainisha hoja inayoonesha udhaifu wa kutafsiri Dini kama "Njia ya mahusiano kati ya mwanadamu na Mungu". Kipengele hiki kiliwapima watahiniwa umahiri wa kuchambua dhana ya Dini kwa mujibu wa Uislamu ambapo watahiniwa mahiri katika dhana hiyo waliweza kuchagua jibu sahihi C *Tafsiri hiyo inaonesha kuwa, Dini ni hiyari kwa wanadamu*. Watahiniwa hao walielewa kuwa kwa mujibu wa tafsiri hiyo mtu anaweza kukataa Dini kwa kudai kuwa haamini kuwepo kwa Mungu.

Aidha, watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi kipengele hiki walionesha kukosa maarifa kuhusu Dhana ya Dini kwa mujibu wa Qur'an. Miongoni mwao walichagua kipotoshi E *Tafsiri hiyo inaonesha kuwa Dini ni lazima kwa wanadamu,* hoja ambayo sio sahihi kwani tafsiri hiyo inatoa uhuru wa mtu kuchagua ama kuwa na Dini au kutokuwa na Dini. Waliochagua kipotoshi A *Zipo njia nyingine za kuhusiana na Mungu tofauti na Dini,* na D *Mwanadamu anahusiana na Mungu kiroho na haitaji Dini,* walishindwa kufahamu kuwa hoja hizo si sahihi kwa sababu zimejengwa katika mtazamo potofu kuhusu dhana ya Mungu na Dini, kwani hakuna namna mwanadamu katika maisha yake

hapa duniani ataweza kuepuka dhana ya kuwa na Mungu na kujitenga na dhana ya Dini. Wengine walichagua kipotoshi B *Tafsiri hiyo imetolewa na jamii ya wasiokuwa Waislamu,* jambo ambalo ni kweli kuwa tafsiri iliyotolewa katika kipengele hiki imetoka kwa jamii ya wasiokuwa Waislamu, hata hivyo ukweli huo haubainishi sababu ya udhaifu wake hivyo halikuwa jibu sahihi. Kwa ujumla, watahiniwa walioshindwa walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya Dini kwa mujibu wa Uislamu.

Kipengele cha (v) mtahiniwa alitakiwa kubainisha jambo ambalo sio lazima kuzingatiwa katika utekelezaji wa Ibada ya Zakat na Sadaqat. Kipengele hiki kiliwapima watahiniwa umahiri wa kuchambua masharti ya utoaji wa Zakat na Sadaka kama yalivyobainishwa na sheria ya Uislamu. Jibu sahihi lilikuwa B *Kutoa mwezi wa Ramadhani,* ambapo watahiniwa weledi katika Zakat na Sadaka waliweza kujibu kwa kuwa ibada ya kutoa kwa ujumla inapaswa kutekelezwa siku zote kwani haifungamani na miezi mahususi.

Watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki, walionesha kutokuwa na maarifa kuhusu masharti ya kutoa katika Uislamu. Hivyo walishindwa kubaini hoja ambayo haikuwa sahihi kutoka katika machaguo waliyopewa. Watahiniwa hao walichagua vipotoshi A *Kutoa vilivyo halali,* C *Kutoa vilivyo vizuri,* D *Kutoa kwa kati na kati* na wengine E *Kujiepusha na Ria.* Hoja zote zilizotajwa katika vipotoshi hivyo ni masharti sahihi yanayopaswa kuzingatiwa katika ibada ya kutoa.

Kipengele cha (vi) mtahiniwa alitakiwa kubaini namna Uislamu unavyomuwezesha muumini kuwa katika Ibada wakati wote wa maisha. Kipengele hiki kilipima uwezo wa kuchambua dhana ya ibada katika Uislamu.Watahiniwa walioelewa vema dhana hiyo waliweza kujibu kwa usahihi kwa kuchagua herufi B *Dhana ya Ibada inahusu kila jambo katika Uislamu.* Watahiniwa hao walielewa kuwa Uislamu umeliweka kila jambo kuwa ni ibada, hivyo mwanadamu akizingatia kufanya kila jambo kwa mujibu wa mafundisho ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake muda wote anakuwa katika ibada.

Watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi kipengele hicho walionesha kukosa maarifa kuhusu dhana ya Ibada katika Uislamu.

Miongoni mwao, walichagua kipotoshi A *Umelazimisha kutekelezwa kwa nguzo tano za Dini*, watahiniwa hao walishindwa kuelewa kuwa utekelezaji wa Nguzo tano za Dini hutumia muda mchache sana katika siku na muda mwingi wa maisha upo nje ya nguzo hizo. Wengine walichagua vipotoshi C *Katika Uislamu kuna Nguzo za Imani*, hoja hii pia haikuwa sahihi kwa kuwa nguzo hizo ni mipaka ya kiitikadi inayoongoza vitendo katika maisha ya muumini hivyo kuwepo kwake tu bila ya utendaji hakusababidhi muumini kuwa katika Ibada. Wengine walichagua kipotoshi D *Uislamu umeondoa uhuru wa watu kupumzika,* ambacho hakikuwa sahihi kwa sababu hata kupumzika pia kwa nujibu wa mafundisho ya Uislamu ni kitendo cha ibada. Vilevile, waliochagua kipotoshi E *Kuna majengo ya Ibada za Waislamu katika nchi zote*, hoja hii haikuwa sahihi kwani sio nchi zote zina majengo ya ibada za Waislamu na pili mwadamu anatumia muda mwingi katika maisha ya kijamii kuliko katika majengo ya ibada.

Kipengele cha (vii) mtahiniwa alitakiwa kubainisha jambo analopaswa kufanya mtu anayemswalia maiti baada ya imamu kuleta takbira ya tatu. Kipengele hiki kilipima umahiri wa watahiniwa kutekeleza Sala ya maiti. Jibu sahihi katika kipengele hiki lilikuwa herufi A *Kumuombea maiti*. Aidha, watahiniwa waliojibu kwa usahihi kipengele hiki walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu utekelezaji wa ibada ya kumsalia maiti hatua kwa hatua hivyo waliweza kuchagua jibu sahihi.

Kwa upande mwingine, baadhi ya watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi baadhi yao walichagua kipotoshi B *Kusoma Surat Fat'ha*, ambalo sio sahihi kwani sura hii husomwa baada ya takbira ya kwanza. Kadhalika, kipotoshi C *Kutia nia,* hakikuwa sahihi kwa sababu nia huletwa moyoni kabla ya Takbira ya kwanza. Vilevile, kipotoshi D *Kusoma Sala ya Mtume,* haikuwa sahihi kwa kuwa kumsalia Mtume ni baada ya Imamu kutamka takbira ya pili. Na mwisho kipotoshi E *Kutoa salaam* hakikuwa sahihi kwa sababu salaam hutolewa baada ya Imam kuleta Takbira ya nne.

Kipengele cha (viii) mtahiniwa alitakiwa kubaini msingi wa Sharia ambao utekelezaji wake unaruhusu ufafanuzi wa mafundisho ya Uislamu kwa mujibu wa mabadiliko ya mazingira na wakati. Kipengele hiki kiliwapima watahiniwa umahiri wa kuchambua misingi ya Sharia katika Uislamu na matumizi yake. Jibu la swali hili lilikuwa herufi A *Ijtihaad,*

ambapo watahiniwa waliojibu kwa usahihi walionesha kuelewa vema msingi huo kuwa ni msingi ambao unahusisha misingi mikuu katika kutafuta suluhisho la mambo kwa kadiri yanavyotokea katika umma.

Aidha, watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki, walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu misingi ya sharia ya Kiislamu kwa ujumla. Baadhi ya watahiniwa hao walichagua kipotoshi B *Qur'an,* C *Sunnah*, D *Qur'an na Sunnah* na Kipotoshi E *Sunnah na Hadith*, walishindwa kuelewa kuwa machaguo hayo hayakuwa sahihi kwa kuwa ndani yake imetajwa misingi mikuu ya sharia katika Uislamu ambayo haina sifa ya kubadilika kutokana na wakati au mazingira.

Kipengele cha (ix) mtahiniwa alitakiwa kubaini muktadha ambao dhana ya Hadithi inafafanuliwa kama jambo au kitu kipya, taarifa au hotuba. Kipengele hiki kiliwapima watahiniwa umahiri wa kuchambua maana ya Hadithi kilugha na kisheria. Jibu sahihi la kipengele hicho lilikuwa herufi C *Katika mazingira ya kilugha*, watahiniwa walioelewa vema mada ya *Sunnah* na Hadithi waliweza kubaini jibu hilo kwa sababu maana hizo hutumiwa kilugha.

Aidha, watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki walichagua kipotoshi B *Kihistoria*, ambalo halikuwa sahihi kwani dhana hiyo haina ufafanuzi tofauti kihistoria. Wengine walichagua kipotoshi A *Katika Mazingira ya Kisheria*, ambalo si sahihi kwa kuwa dhana ya Hadithi kisheria ni simulizi juu ya *Sunnah* ya Mtume (S.A.W). Vilevile wapo wanafunzi waliochagua kipotoshi D *Kimatumizi*, watahiniwa hao walishindwa kuelewa kuwa matumizi ya dhana ya Hadithi yanatofautiana baina ya watu na kipotoshi hiki hakielezi muktadha mahususi wa matumizi hayo, hivyo halikuwa jibu sahihi. Aidha, waliochagua kipotoshi E *Katika kuifafanua Sunna* walishindwa kuelewa kuwa dhana ya Hadithi ikitumika katika kuifafanua Sunna ni sawa na inavyotumika kisheria. Kwa ujumla, watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi kipengele hiki hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana ya *Sunnah* na *Hadithi.*

Katika kipengele cha (x) mtahiniwa alitakiwa kubaini mafundisho mahususi yanayopatikana katika Surat Ikhlas. Kipengele hiki kilipima watahiniwa umahiri wa kuchambua mafunzo ya sura mbalimbali za

Qur'an katika sura zilizochaguliwa. Watahiniwa weledi wa mafunzo ya sura zilizochaguliwa walichagua jibu E *Allah (S.W) ndiyo jina la Dhati la Mwenyezi Mungu,* watahiniwa hao walielewa kuwa Surat Ikhlas ndio sura kuu ambao imebeba mudhui makubwa kuhusu wasifu wa Mwenyezi Mungu (S.W) hivyo waliweza kubaini jibu sahihi la kipengele hiki.

Ama, watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi walionesha kukosa maarifa ya kutosha kuhusu mafunzo mahususi yanayopatikana katika Suratul-Ikhlas na sura zingine zilizochaguliwa. Baadhi ya watahiniwa hao walichagua herufi A *Shetani ni adui mkubwa wa Mwenyezi Mungu* na kipotoshi D *Kazi kubwa ya Shetani ni kutia wasiwasi moyoni.* Vipotoshi hivo havikuwa sahihi kwa sababu hoja zake zilikuwa ni mafunzo yanayopatikana katika Surat Nnas. Wengine walichagua kipotoshi B *Kuna sharia katika giza la usiku linapoingia*, ambao ni ujumbe unaopatikana katika Surat Falaq. Aidha, waliochagua kipotoshi C *Uislamu ni njia sahihi ya maisha,* walishindwa kuelewa kwamba mafunzo hayo yanapatikana katika Surat Fat'ha.

Kipengele cha (xi) mtahiniwa alitakiwa kubaini jambo linaloonesha wajibu wa mwanadamu kutafuta Dini sahihi katika maisha yake. Swali lilipima umahiri wa kutathmini wajibu wa mwanadamu kutafuta dini sahihi katika maisha yake. Aidha, watahiniwa weledi katika dhana ya Dini Sahihi walijibu kipengele hiki kwa kuchagua herufi D *Kuletwa kwa Mitume wa Mungu.* Hoja hiyo ilionesha wajibu wa mwanadamu kutafuta Dini kwa sababu ilikuwa ni kawaida kwa Mwenyezi Mungu (S.W) kabla ya kuletwa Mtume Muhammad (S.A.W) kuleta wajumbe wake kila baada ya muda ili kuwajulisha watu njia sahihi ya maisha.

Watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki, baadhi yao walichagua kipotoshi A *Kuwepo kwa dini nyingi duniani,* hoja ambayo haikuwa sahihi kwa sababu wingi wa dini unaongeza uwezekano wa watu kupotea zaidi ikiwa watatafuta iliyo sahihi kwa mitazamo yao. Watahiniwa wengine walichagua kipotoshi B *Hitajio la mwanadamu kiroho,* ambalo halikuwa sahihi kwa sababu hitajio hili linaweza kutoshelezwa hata katika dini zisizo sahihi na ili aweze kupata usahihi atahitaji muongozo. Wapo wengine waliochagua kipotoshi C *Uwezo wa mwanadamu kuamua,* ambalo pia halikuwa sahihi kwa kuwa maamuzi ya mwanadamu yanaendeshwa na utashi wa nafsi yake ambao

hauwezi kumuelekeza kupata dini sahihi. Ama waliochagua kipotoshi E *Kuwepo kwa midahalo ya kidini*, hawakuwa sahihi kwa sababu hata dini potofu pia zinawatetezi hivyo bado mwanadamu atahitaji mwongozo katika kutafuta usahihi. Watahiniwa waliochagua vipotoshi hivo walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu Dini sahihi anayostahiki Mwanadamu.

Kipengele cha (xii) mtahiniwa alitakiwa kubaini malengo makubwa ya kuumbwa maumbile yote yaliyomzunguka mwanadamu hapa duniani kwa mujibu wa Uislamu. Kipengele hiki kiliwapima watahiniwa umahiri wa kukumbuka malengo makuu na madogo ya maumbile yote yaliyomzunguka mwanadamu. Watahiniwa waliokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu Historia katika Uislamu. Dhana juu ya Historia walichagua jibu sahihi D *Kumtumikia mwanadamu kimahitaji,* watahiniwa hao walielewa kuwa Mwenyezi Mungu (S.W) amevifanya vitu vyote kuwa vitiifu kwa mwanadamu ili aweze kuvitumia.

Watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi kipengele hiki baadhi yao walichagua kipotoshi C *Kuonesha uwezo wa kiuumbaji,* A *Kuipamba Dunia na Anga* na B *Kuweka usawa wa Kiekolojia.* Watahiniwa hao walishindwa kuelewa kuwa hoja hizo hazielezi malengo makuu ya kuumbwa kwa maumbile mengine ingawa mambo hayo yanatimiza yote yaliyotajwa. Wengine walichagua kipotoshi E *Kuwa alama kwa malaika na watu,* ambalo pia halikuwa sahihi kwani malaika hawahitaji maumbile yaliyotuzunguka kwa kazi hiyo. Kwa ujumla watahiniwa walioshindwa walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Historia katika Uislamu.

Katika kipengele cha (xiii) mtahiniwa alitakiwa kubainisha lengo kuu la kusoma historia kiutendaji. Kipengele hiki kilipima umahiri wa kuchambua malengo ya Historia kama yanavyobainishwa na Uislamu. Watahiniwa hodari katika mada ya Historia katika Uislamu walichagua jibu sahihi C *Kupata mafunzo na kujirekebisha*, watahiniwa hao walielewa vema kuwa malengo ya historia sio kukumbuka matukio yaliyopita bali ni kutoa mafunzo kutoka katika matukio hayo mafunzo yatakayosaidia kurekebisha wakati uliopo na kuchukua tahadhari kwa wakati ujao.

Aidha, watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Historia katika Uislamu hivyo walishindwa kubaini malengo yake kiutendaji. Baadhi ya watahiniwa hao walichagua vipotoshi A *Kuona asili na hadhi yetu,* B *Kujikumbusha yaliyopita*, D *Kuona neema mbalimbali tulizopewa,* na kipotoshi E *Kuonesha madhara ya kumuasi mungu.* Vipotoshi hivo vyote vilieleza malengo madago ya Historia hivyo havikuwa majibu sahihi.

Kipengele cha (xiv) mtahiniwa alitakiwa kubaini sababu ya Mtume (S.A.W) kuwaamrisha Maswahaba wake kuhama kutoka Makka kwenda Madina mwaka wa 13 B.U. Kipengele hiki kilipima umahiri wa kuchambua historia ya Hijrah ya Mtume (S.A.W) na Maswaba wake kuelekea Madinah. Aidha, watahiniwa weledi wa historia ya Hijrah waliweza kubaini sababu hiyo na kuchagua jibu sahihi D *Hitimisho la mikataba ya Aqaba baina ya Waislamu na watu wa Madina*, watahiniwa hao walielewa kuwa mikataba miwili ya Aqaba ilibainisha kwa wakati tukio la hilo na kwa taufiki ya Mwenyezi Mungu tukio hilo likakamilika.

Watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya historia ya kulingania Uislamu Makka. Baadhi ya watahiniwa hao walichagua kipotoshi A *Kufunguka kwa hali ya kibiashara katika mji wa Madina wakati huo,* na E *Kuongezeka kwa ushindani wa kibiashara katika mji wa Makka.* Hoja hii hayakuwa sahihi kwa sababu tukio la Hijra halikusababishwa na mazingira ya kibiashara. Wengine walichagua herufi B *Hitaji la Waislamu kupata sehemu nzuri ya kuishi kwa amani na utulivu*, hoja hii haikuwa sahihi kwa Hijrah ya Madinah bali liliakisi tukio la Hijrah Habasha (Ethiopia).

Watahiniwa wengine walichagua herufi C *Hitaji la Waislamu kuishi katika sehemu yenye huduma nzuri za kijamii,* hoja ambayo haikuwa sahihi pia kwani kihistoria mji wa Makka ulikuwa na huduma nyingi za kijamii kuliko Madinah wakati Waislamu wanafanya Hijrrah.

Kipengele cha (xv) mtahiniwa alitakiwa kuonesha mtiririko sahihi unaobainisha ujumbe wa Mwenyezi Mungu (S.W) kwa Mtume wake (S.A.W), uliokusudia kumuandaa kimafunzo. Kipengele hiki kilipima umahiri wa kukumbuka historia ya maandalizi ya Mtume (S.A.W) kimafunzo. Aidha, watahiniwa weledi wa historia hiyo walichagua jibu


C *Surat Alaq, Surat Muzammil na Surat Muddathir*. Watahiniwa hao walionesha kukumbuka vema matukio muhimu katika maandalizi ya kimafunzo ya Mtume (S.A.W) na kuyaunganisha katika mtiririko sahihi.

Watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hicho hawakuwa na maarifa ya kutosha katika kipengele cha maandalizi ya Mtume (S.A.W) kimafunzo, hivyo walichagua majibu yao kwa kukisia. Baadhi yao walichagua kipotoshi A *Surat Alaq, Surat Fat'ha na Surat Muddathir,* B *Surat Alaq, Surat Muddathir na Surat Muzammil,* ambavyo havikuwa sahihi kwa sababu ndani yake kuna Surat Fat'ha haipo katika sura za maandalizi ya Mtume (S.A.W) kimafunzo. Wengine walichagua kipotoshi D *Surat Alaq, Surat Muzammil na Surat Fat'ha,* na kipotoshi E *Surat Muzzammil, Surat Alaq na Surat Mudathir*, vipotoshi hivi havikuwa sahihi kwa kuwa havikuzingatia mtiririko sahihi.

### 2.1.2 Swali la 2: Nguzo za Uislamu

Swali hili lilitolewa kutoka mada ndogo ya *Funga* za *Sunnah*, na lilipima watahiniwa umahiri wa kuelewa Funga mbalimbali za Sunnah na nyakati zake. Aidha, mtahiniwa alitakiwa kuoanisha Funga za Sunnah zilizotajwa katika orodha A (i) - (v) na majina ya Funga yaliyowekwa katika orodha B (A) – (G) kisha kuandika herufi ya jibu sahihi kwa kila kipengele katika kijitabu chake cha kujibia.

Swali lilijibiwa na watahiniwa wote 84,230 (100%) waliofanya mtihani. Kati yao watahiniwa 37,625 (44.67%) walipata alama 0 hadi 4 ambao ni ufaulu dhaifu na watahiniwa 36,373 (43.18%) walipata alama 5 hadi 8 ambao ni ufaulu wa wastani. Aidha, watahiniwa 10,232 (12.15%) walipata alama 9 hadi 15 ambao ni ufaulu mzuri. Chati Na. 2. inaonesha muhtasari wa ufaulu wa watahiniwa hao kwa asilimia.




**Chati Na. 2:** *Asilimia ya ufaulu wa watahiniwa katika swali la 2*

Chati Na. 2 inaonesha kuwepo kwa ufaulu wa wastani katika swali kwa kuwa asilimia 55.33 ya watahiniwa walipata alama 3 hadi 5 ikilinganishwa na asilimia 44.67 ya watahiniwa walio na ufaulu dhaifu.

Watahiniwa waliofaulu walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu Nguzo za Uislamu hususani *Funga* za *Sunnah,* hivyo waliweza kuoanisha kwa usahihi vipengele vitatu hadi vitano.

Katika kipengele cha (i) mtahiniwa alitakiwa kubaini jina la Funga inayotekelezwa siku za tarehe 12, 13 na 14 katika miezi ya Hijriya, ambapo jibu sahihi la kipengele hiki lilikuwa herufi C *Funga siku nyeupe*, watahiniwa waliochagua jibu hili walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu Funga za Sunnah. Aidha, watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi wengi wao walichagua herufi G *Masiku Meusi*. Watahiniwa hao walishindwa kubaini kuwa katika Uislamu hakuna Funga za Sunnah za siku nyeusi na tarehe hizo katika mwezi muandano hazisadifu kuwa nyeusi. Wengine walichagua kipotoshi F *Siku ya Arafa*, ambapo walishindwa kutambua kuwa Funga ya Arafa inapatikana katika mwezi Dhulhijja pekee na si miezi yote. Pia, wapo waliochagua herufi E *Sitta Shawwal.* Walishindwa kuelewa kuwa *Shawwal* (*Mfungo Mosi*) hutokea mwezi wa 10 Hijria. Pia, watahiniwa wachache walichagua vipotoshi A *Funga ya Ashura*, B *Funga ya Kafara* na D *Sunna Nabii Daud*. Walichagua majibu hayo kutokana na kutokuwa na maarifa ya kutosha juu ya Funga za Sunnah.

Kipengele cha (ii) mtahiniwa alitakiwa kubaini jina la Funga inayotekelezwa siku ya tarehe 9 katika mwezi wa Dhul Hijja. Watahiniwa waliojibu vema kipengele hiki walichagua jibu F *Funga ya Arafa.* Watahiniwa hao waliweza kuikumbuka vema Funga ya Arafah kutokana na umuhimu na umashuhuri wake. Aidha, watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi baadhi yao walichagua herufi E *Sitta Shawwal* ambayo haikuwa sahihi kwa kuwa *Sitta Shawwal* inapatikana katika mwezi wa Shawwal (wa kumi) katika miezi ya Kiislamu. Kadhalika, wengine walichagua herufi A *Funga ya Ashura,* ambayo pia haikuwa sahihi kwa sababu Funga hiyo inapatikana katika mwezi Muharram. Wengine walichagua C *Funga Siku nyeupe*, ambayo pia haikuwa sahihi kwani Funga ya siku nyeupe inajumuisha tarehe tatu ambazo ni 12, 13 na 14 ya kila mwezi wa kiislamu.

Katika kipengele cha (iii) mtahiniwa alitakiwa kubaini jina la Funga inayopatikana siku ya tarehe 10 katika mwezi wa Muharram. Watahiniwa waliokumbuka vema jina la funga hiyo walichagua herufi A *Funga ya Ashura,* ambayo ni siku muhimu ya kihistoria kwa kuwa imeambatana siku ya ukombozi wa watu wa Israeli wakiwa na Nabii Musa (A.S) dhidi ya Firauni. Wengine walichagua herufi C *Funga siku nyeupe* ambayo haikuwa sahihi kwani siku nyeupe zinaanza tarehe 12 sio 10.

Katika kipengele cha (iv) mtahiniwa alitakiwa kubaini Funga *muakkada* kila mwezi wa 10 Hijiria, ambapo jibu lake lilikuwa herufi E *Sitta Shawwal,* Funga hiyo ni muakkada kwani Mtume (S.A.W) hakuwahi kuiacha. Ama watahiniwa waliochagua jibu hilo walielewa vema Funga hiyo hivyo waliweza kuoanisha kwa usahihi. Aidha, watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi, baadhi yao walichagua herufi A *Funga ya Ashura,* watahiniwa hao walichanganya na Funga hii kwa kuwa inatekelezwa tarehe 10 Muharram wakati *Sitta Shawwal* inatekelezwa Mwezi wa 10. Wengine walichagua herufi D *Sunnah Nabii Daud* , ambapo walidhihirisha kutokuwa na maarifa kuhusu Funga za Sunnah kwani Funga ya Nabii Dawud haina miezi maalumu ukitoa mwezi wa Ramadhani.

Kipengele cha (v) mtahiniwa alitakiwa kubaini jina la Funga ya Sunna inayotekelezwa kila baada ya siku moja. Watahiniwa waliofahamu vema Funga za *Sunnah* walichagua jibu sahihi D *Sunna Nabii Dawud*, kwani

Funga hii ni ya kipekee kwa watu wanaopenda kudumu na ibada ya Funga. Aidha, watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi, baadhi yao walichagua kipotoshi B *Funga ya kafara,* ambayo si sahihi kwani Sunna hiyo ni matokeo ya makosa ya mtu na juhudi za kuutafuta uchamungu. Wengine walichagua herufi C *Funga ya siku nyeupe na* ambayo si sahihi kwa Funga ya siku nyeupe zinatekelezwa kwa mfululizo kuanzia tarehe 12 hadi 14 ya kila mwezi isipokuwa Ramadhani.

Kwa ujumla katika swali hili watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi walionesha ukosefu wa maarifa ya kutosha na wengine kutokuwa na maarifa kabisa kuhusu Funga za Sunna.


## 2.2 SEHEMU B: Majibu Mafupi

Sehemu hii ilikuwa na maswali saba ya majibu mafupi, kutoka mada za *Qur'an, Nguzo za Imani, Familia ya Kiislamu, Historia ya Uislamu baada ya Kutawafu Mtume (S.A.W), Fiqh, Mfumo wa jamii ya Kiislamu na Dini sahihi anayostahiki Mwanadamu.* Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote, ambapo kila swali lilikuwa na alama tano (5) hivyo, jumla ya alama zote zilikuwa 35.

### 2.2.1 Swali la 3: Qur'an

Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kutumia hoja tano kubainisha udhaifu wa madai kuwa Mtume (S.A.W) alifundishwa Qur'an na watu. Swali hili lilipima umahiri wa kuchambua ithibati ya Qur'an kuwa ni maneno na kitabu cha Allah (S.W).


Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa 84,230 (100%) walifanya swali hili, ambapo kati yao watahiniwa 46,201 (54.85%) walipata alama 0 hadi 1.5 ambao ni ufaulu dhaifu. Watahiniwa 28,797 (34.19%) walipata alama 2 hadi 3.5 ambao ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 9,232 (10.96%) walipata alama 4 hadi 5 ambao ni ufaulu mzuri. Muhtasari wa ufaulu wa watahiniwa hao kwa asilimia ni kama unavyoonekana katika Chati Na. 3.




**Chati Na. 3:** *Asilimia ya ufaulu wa watahiniwa katika swali la 3*

Chati Na. 3 inaonesha kuwa ufaulu wa watahiniwa katika swali ulikuwa wa wastani kwa kuwa asilimia 45.15 walipata alama 2 hadi 5 ukilinganisha na asilimia 54.85 waliopata ufaulu dhaifu. Aidha, sababu za ufaulu huu zimefafanuliwa kama ifutavyo;

Uchambuzi uliofanyika katika majibu ya watahiniwa waliofaulu umeonesha kuwa, watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu Qur'an na walielewa vema matakwa ya swali. Aidha, katika majibu yao walieleza hoja mbalimbali zinazoonesha udhaifu wa madai kuwa Mtume (S.A.W) alifundishwa Qur'an na watu. Miongoni mwa hoja hizo ni pamoja na: (i) *Mtume (S.A.W) hakuwa anajua kusoma wala kuandika, hivyo hapakuwa na uwezekano wa kuwa alifundishwa Qur'an na watu,* (ii) *Kama ni kweli walikuwepo waliomfundisha Mtume (S.A.W) walipaswa kuwa wajuzi zaidi ya yeye aliyefundisha lakini mpaka sasa hakuna mtu mwenye sifa hizo,* (iii) *Lugha ya Qur'an haikuwa inaeleweka wazi kwa wengi kati yao kwa hivyo hapakuwa na uhusiano wa Mtume kufundishwa Qur'an na yeyote miongoni mwao wala mtu mgeni,* (iv) *Mafundisho ya Qur'an kupingana na vitabu vingine, kuna tofauti kubwa kati ya Qur'an na vitabu vingine vya dini, jambo ambalo halikutegemewa kuwepo kama Mtume (S.A.W) alifundishwa Qur'an na watu,* (v) *Uwiano uliopo katika Qur'an kihesabu na matukio haijawahi kutokea kitabu chochote kilichoandikwa na binadamu kuwa hivyo, mfano idadi ya Basmallah ni 114, neno yawm kurudiwa mara 365, Shahari mara 12 na mengineyo na* (vi) *Madai hayo kupingana na ukweli wa kihistoria kuhusu maisha ya Mtume (S.A.W).* Kielelezo Na. 3.1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali hili.


3. i). Mtume (s.a.w) alifundishwa Qur'an na malaika Jibril (a.s)
ii). Qur'an yenyewe inajieleza kuwa ni maneno ya Allah (s.w)
iii). Hakuna mwanaadamu yeyote aliyeweza kutunga kitabu mithili ya Qur'an
iv). Mpangilio wenyewe wa Qur'an kabla mas-hafu.
v). Qur'an kushuka kidogokidogo kwa kipindi cha miaka 23.

Kielelezo Na. 3.1: Sampuli ya majibu sahihi ya swali la 3

Uchambuzi zaidi umeonesha kuwa waliopata alama hafifu (54.85%) walikosa maarifa ya kutosha kuhusu ithibati ya Qur’an kuwa ni kitabu cha Mwenyezi Mungu na wengine walishindwa kubaini matakwa ya swali hilo. Sababu hizo zimejitokeza kulingana na aina ya majibu yaliyotolewa na watahiniwa hao katika kujibu swali hili.


Baadhi ya watahiniwa walieleza hoja za kuhifadhiwa Qur’an badala ya kubainisha udhaifu wa madai kuwa Mtume (S.A.W) alifundishwa Qur’an na watu, watahiniwa hao waliandika; *Mtume alihifadhishwa Qur’an kichwani na Malaika Jibril, Mtume kuwasomea waandishi wapatao 42, Mtume akawaambia wapange aya hizo kama inavyotakiwa, Mtume aliambiwa wamsomee ili kuhakiki na Mtume alihifadhisha maswahaba Qur’an vifauani mwao.*Wengine walieleza; *Kulazimishwa kusoma Qur’an na malaika Jibril ili aweze kusoma Qur’an, kuwasomea maswahaba zake Qur’an ili wahifadhi katika vifua vyao na isije ikapotea, kuwafundisha kuisoma maswahaba zake ili waweze kuijua na kuiandika, kuifasiri kuwa ina maana gani kwa watu wake ili waweze kuijua na kushuka pale ambapo pana hitajio la Qur’an pamoja na kuweza kuwasomea watu wake.* Majibu ya watahiniwa hao yaliashiria kutoelewa matakwa ya swali husika hivyo badala ya kutoa hoja zinazobainisha udhaifu wakaeleza njia zilizotumika kuihifadhi Qur’an.

Aidha, watahiniwa wengine walitaja madai mengine ya makafiri dhidi ya Qur’n, kama vile; *Dai kuwa Qur’an ni mashairi aliyoyatunga Mtume (S.A.W), Mtume (S.A.W) ni mwendawazimu, Muhammad ni kifafa na Qur’an ni njozi zilizovurugika* badala ya kubainisha udhaifu wa madai ya Mtume (S.A.W) kufundishwa Qur’an na watu. Mwingine aliandika madai yasiyo sahihi kwa makafiri kama vile:- *Watu waliamini kuwa Mtume amefundishwa Qur’an na watu kwa kuwa baadhi ya vitu alikuwa hajavijua vizuri, waliamini kuwa Mtume (S.W) ndiye yeye aliyeanzisha*

*Itikadi kuwa Qur'an kaianzisha yeye mwenyewe, waliamini maneno ambayo alikuwa akiwaambia watu yametoka kwa mtu ambaye alikuwa akimfundisha kwa kuwa na mafunzo na maonyo mbalimbali, waliamini kuwa Mtume alikuwa akifundishwa na mtu kwa kuwa alikuwa hajaikalili vizuri Qur'an na waliamini kuwa maneno aliyokuwa akiwaambia watu yaliyokuwa katika Qur'an kuwa amejitungia ili kuwapotosha kwa hivyo watu waliamini kuwa Mtume Muhammad (S.W.A) kuwa amefundishwa tu na mtu.* Maelezo hayo yaliashiria kukosa maarifa kuhusu ithibati ya Qur'an hivyo walikwenda kinyume na matakwa ya swali.

Baadhi ya watahiniwa, walitaja njia anazotumia Mwenyezi Mungu (S.W) kuwasiliana na waja wake kama vile: *Kupitia nyuma ya pazia, kupitia Wahy, kupitia ndoto za kweli, kupitia maandishi pamoja na kupitia malaika.* Wengine walieleza: *Walisema kuwa Mtume hana elimu ya kutosha, si Mtume wa Allah, hawatofata muongozo wake, Mtume wa uongo, Mtume hana ujuzi juu ya Qur'an.* Wengine walijibu; *Hawajui swala zima kuhusiana na Qur'an, hawajui kuna Mungu muumba anayeumba kila kitu katika hii dunia, hawajui hadhi ya Mtume (S.A.W) kwa watu waliopo ardhini, hawawazi Qur'an ameishusha Mwenyezi Mungu kumpelekea Mtume wake kwa ajili ya kuja kuwaelimisha dini na wanapuuza mawazo yao finyu yasiyo na maana kwa watu katika ulimwengu huu hasa wa sasa.* Watahiniwa hao walionesha kukosa maarifa ya kutosha kuhusu Qur'an hivyo, walieleza mambo yaliyo nje na matakwa ya swali.

Kwa ujumla, watahiniwa wengi walioshindwa kujibu kwa usahihi swali hili, walishindwa kubaini matakwa ya swali na wengine walikosa maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Qur'an. Kielelezo Na. 3.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi katika swali hili.


3. (i) Watu waliamini kuwa mtume amefundishwa qur an na watu kwa kuwa baadhi ya vitu alikua hajavijua vizuri
(ii) Waliamini kuwa mtume (S.w) ndiye yeye aliyetanzisha itikadi kuwa qur an kaianzisha yeye mwenyewe
(iii) Waliamini maneno ambayo alikuwa akiwaambia watu yametoka kwa ~~two~~ mtu ambaye alikua akimfundisha kwa kuwapa mafunzo na maonyo mbalimbali
(iv) Waliamini kuwa mtume alikua akifundishwa na mtu kwa kuwa alikuwa hajaikahili vizuri qur an
(v) Waliamini kuwa maneno aliyokuwa akiwaambia watu ~~am~~ yaliyokuwa katika qur ani kuwa ameyatungia ili kuwapotosha kwa hiyo watu waliamini kuwa mtume muhamadi (S.w.a) kuwa amefundishwa tu na mtu


Kielelezo Na. 3.1: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 3

Katika kielelezo Na 3.1 mtahiniwa ametoa hoja za kubuni dhidi ya makafiri badala ya kuonesha udhaifu wa madai yao kuwa Mtume (S.A.W) alifundishwa Qur’an na watu.

### 2.2.2 Swali la 4: Nguzo za Imani

Swali hili lilitoka katika mada ndogo ya Kuamini Qadar ya Mwenyezi Mungu, ambapo mtahiniwa alitakiwa kutumia hoja mbili kumuelimisha mtu ambaye anafanya maovu hadharani na kudai kuwa ni Qadar ya Mwenyezi Mungu (S.W). Swali hili lilipima umahiri wa watahiniwa kutumia maarifa ya dhana ya Qadar katika kuelimisha jamii.

Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa wote 84,230 (100%) walifanya swali hili. Kati yao, watahiniwa 74,448 (88.39%) walipata alama 0 hadi 1.5 ambao ni ufaulu dhafifu. Watahiniwa 8,915 (10.58%) walipata 2 hadi 3.5 ambao ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 867 (1.03%) walipata alama 4 hadi 5 ambao ni ufaulu mzuri. Muhtasari wa ufaulu wa watahiniwa hao ni kama unavyoonekana katika Chati Na. 4.




**Chati Na. 4:** Asilimia ya ufaulu wa watahiniwa katika swali la 4

Chati Na. 4 inaonesha kuwa, ufaulu wa jumla katika swali hili ulikuwa dhaifu kwani asilimia 88.39 ya watahiniwa walipata alama 0 hadi 1.5 ikilinganishwa na asilimia 11.61 waliofaulu.


Uchambuzi uliofanyika katika majibu ya watahiniwa umeonesha kuwa, ufaulu dhaifu katika swali hili ulichangiwa na watahiniwa kukosa maarifa ya kutosha kuhusu nguzo ya sita ya imani ya Kiislamu. Vile vile, baadhi ya watahiniwa kushindwa kubaini matakwa ya swali, hali hiyo ilisababisha watahiniwa hao kushindwa kujibu swali hili ipasavyo.

Miongoni mwa majibu waliyotoa ni kama vile; *Maovu ni chanzo kikubwa cha kumuingiza motoni na maovu ni chanzo kikubwa cha matatizo katika jamii,* mwingine akaandika: *Kufanya hivyo kutapelekea kumuasi Allah na Mtume wake, hivyo hilo jambo sio sahihi kulifanya, halitakiwi kufanywa na pia kufanya hivo kutapelekea kutokuwa na mashirikiano na Waislamu. Kwani utakapo kuwa tayari ushaasirika na utandawazi basi Waislamu watakutenga katika jamii*. Majibu haya yaliashiria kuwa watahiniwa hao walishindwa kubaini matakwa ya swali, hivyo walieleza matokeo ya matendo maovu kwa mtu binafsi na kwa jamii.

Watahiniwa wengine waliandika; *Qadar ni makadirio juu ya jambo fulani wala sio kupanga maovu mbele za hadhara na kufanya maovu huku anachekea ataingia motoni huku analia.* Pia, wapo waliojibu*: Kufanya maovu ni kukiuka maamrisho ya Allah (S.W) na Mitume wake*

*na kufanya kwa makusudi sio lengo kuu la kuumbwa kwa binadamu* na wengine walijibu: *Uelewa wa kulifanya baya na jema ukishalijua inakuwa si Qadar na pia Qadar haifanywi makusudi*. Mtahiniwa mmoja alijibu: *Ni kuvunja amri ya Allah pamoja na kuvunja mwanadamu katika uumba ili kuja kuwa Mcha Mungu*. Majibu haya yalionesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu Kuamini Qadar ya Mwenyezi Mungu.

Watahiniwa wengine walieleza Qadar kama jambo la uovu linalotendwa katika jamii, badala ya kuelimisha ufahamu potofu juu ya dhana hiyo. Watahiniwa hao waliandika; *Qadar hairuhusiwi kufanya maovu hadharani kwa kuwa ni Qadar kwani yeyote atakayefanya maovu kwa Qadar basi atakuwa ni mwenye kupata dhambi na pia Qadar hairuhusiwi kwa Waislamu kwani ni mojawapo ya uvunjaji wa sheria na taratibu za Kiislamu.* Wengine waliandika lengo la kuumbwa mwanadamu pamoja na lengo la funga ambayo yote ni kinyume na matakwa ya swali. Watahiniwa hao waliandika; *Mwenyezi Mungu amemuumba mwanadamu ili amuabudu na siyo kumuasi na lengo la kuletwa funga ni kusamehewa wala siyo Qadar ya maovu.* Majibu hayo dhaifu ya watahiniwa katika swali hili yaliashiria kutokuwa na maarifa kuhusu dhana ya Qadar. Kielelezo Na. 4.1 kinaonesha sampuli ya maelezo ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi.



4. i) Maovu ni chanzo kikubwa cha kumuingiza motoni, kwa sababu maovu ni hali ambayo inamchukiza Allah (s.w) hata kama ni Qadar hali ambayo inapelekea kupata adhabu kali sana. Kwa kuwa madai yake ni Qadar na Qadar ni uwezo wa Allah (s.w) ni sawa lakini maovu kwa makusudi hapo hakuna Qadar tena ni kujiendeleza tu.

ii) Maovu ni chanzo kikubwa cha matatizo katika jamii, hali ambayo inapelekea kuchafuka kwa jamii hata kama ni Qadar hatukatai lakini huyu ndugu masudi yeye kakosea tena sana hivyo basi suluhisho ni kuachana na maovu kwa sababu huenda alijisahau na sasa amekumbushwa akirudia tena Allah (s.w) hatomuangali.

Kielelezo Na. 4.1: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 4

Katika kielelezo namba 4.1 mtahiniwa alishindwa kuelimisha dhidi ya mtazamo potofu juu ya Qadar badala yake alieleza matokeo ya kutenda mambo maovu.

Licha ya watahiniwa wengi (88.39%) kupata alama za chini katika swali hili, walikuwepo wachache (11.61%) waliofaulu. Watahiniwa hao walibaini matakwa ya swali husika na kutumia maarifa yao kujibu swali hilo ingawa si kwa ukamilifu. Aidha, majibu kamili ya swali hili yalikuwa; (*i) Katika mambo ambayo mwanadamu ana uhuru nayo, Allah (S.W) kamuachia afanye kwa uhuru wake (ii) Mwanadamu amepewa mwongozo na akili, vipaji na uwezo wa kubaini mema na maovu na kufahamu faida ya kutenda mema na madhara ya kutenda maovu (iii) Qadar ni mpango wa siri wa Mwenyezi Mungu (S.A.W) na hakuna anayejua hata anayefanya uovu pia haijui hivyo mtu atahukumiwa kwa anayoyadhihirisha.* Kielelezo Na. 4.2 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa.


4 (i) Binaadamu tumetunukiwa akili na milango ya fahamu ambayo inatuwezesha kuwa na utambuzi kuhusiana na mambo mema na mabaya. Hivyo haifai kusema ni Qadar wakati ambapo sisi ni wajuzi wa mema na maovu.
(ii) Pia, kutunukiwa elimu ambayo inatufanya tuwe na machaguo ya matendo yetu. Hivyo kusema ni Qadar ni makosa kwa kuwa elimu yetu (Qur-an) ilikwisha eleza kuhusu yale ambayo tunatakiwa kuyafanya na yale makatazo tunayotakiwa kuachana nayo.


Kielelezo Na. 4.1 Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefaulu katika swali la 4

### 2.2.3 Swali la 5: Familia ya Kiislamu

Swali hili lilitoka katika mada ndogo ya Ndoa katika Uislamu, mtahiniwa alitakiwa kupendekeza njia zitakazowezesha taasisi ya ndoa katika jamii ya sasa kufikia malengo yake kimalezi na kuimarisha maadili mema kwa watoto. Swali lilipima watahiniwa umahiri wa

kuunda hoja zinazobainisha njia zitakazowezesha taasisi ya ndoa kufikia malengo yake kimalezi na kuimarisha maadili katika jamii.

Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa 84,230 (100%) waliofanya mtihani walifanya swali hili. Kati yao watahiniwa 47,129 (55.95%) walipata alama 0 hadi 1.5 ambao ni ufaulu dhaifu. Watahiniwa 30,631 (36.37%) walipata alama 2 hadi 3.5 ambao ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 6,470 (7.68%) walipata alama 4 hadi 5 ambao ni ufaulu mzuri. Chati Na. 5 inaonesha muhtasari wa ufaulu wa watahiniwa hao kwa asilimia.





**Chati Na. 5:** Asilimia ya ufaulu wa watahiniwa katika swali la 5

Chati Na. 5 inaonesha kuwa ufaulu wa watahiniwa katika swali ulikuwa wa wastani kwa kuwa asilimia 44.05 ya watahiniwa walipata alama 2 hadi 5. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu Ndoa katika Uislamu na malengo yake kwa ujumla na walielewa vema matakwa ya swali.

Aidha, watahiniwa hao walitoa njia mbalimbali zilizojibu swali hilo kama vile; (i) *Kuwekeza katika mafundisho ya kimuongozo (Uislamu) katika hatua zote za makuzi (malezi) ya watoto tokea kuzaliwa kwake hadi kujitegemea, (ii)kuimarisha ushirikiano baina ya baba na mama na kuonyesha mfano wa tabia njema, kwa kuwa watoto wanajifunza zaidi kwa kuona kuliko kusikia,(iii) kuimarisha ushirikiano baina ya majirani ili kurudisha ushiriki wa pamoja katika kulea kizazi,(iv)kuondoa ushindani katika kivuli cha dhana ya usawa baina ya baba na mama*


*katika usimamizi wa malezi ya watoto (wazazi kuzingatia wajibu wao), (v)kufungua milango ya ukaribu na mazungumzo baina ya wazazi na watoto* pamoja na (vi) *Wanawake kurudi katika kazi na wajibu wao wa asili (kimaumbile) katika kukilea kizazi.* Kielelezo Na. 5.1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali hilo.


5. Kwa kuwaamrisha mema na kuwakataza maovu
- Kwa kuwahamasisha Wamche Allah (s.w)
- Kwa kuwafatilia mienendo ya ya kila siku
- Kwa kuwafundisha dini
- kwa kujenga mila na kusikiliza changamoto zinazowakumba

Kielelezo Na. 5.1: Sampuli majibu sahihi ya swali la 5

Uchambuzi zaidi uliofanyika katika majibu ya watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi swali hili ulibaini kuwa, watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Ndoa katika Uislamu na wengine walishindwa kubaini matakwa ya swali. Miongoni mwao walitaja taasisi zinazosimamia maadili katika jamii kama vile: *Kupitia mahakama, kimila na desturi, kupitia dini na ndoa za mitala.* Wengine walieleza misingi ya *Fiqh* badala ya kutoa njia zitakazowezesha taasisi ya ndoa kufikia malengo yake kimalezi, watahiniwa hao walitaja; *Sunnah, Qur'an, Hadith na Ijtihad.* Wengine walitaja njia za uzazi wa mpango kama vile: *Njia ya kutumia kalenda ya uzazi, kutumia vitanzi pamoja na kufunga kizazi kwa mwanamke au mwanaume,* majibu hayo yaliashiria kukosa maarifa kuhusu Ndoa katika Uislamu.

Kwa upande mwingine, baadhi ya watahiniwa walitaja masharti ya Ndoa kama vile: *Mume awe baleghe na azingatie masharti ya ndoa na mke nae azingatie, pawe na walii, pawe na ijabu na kabuli, pawe na idhini ya mke na mume awe muislamu na mke*. Mwingine alieleza hekima ya kuoa mke zaidi ya mmoja, kama vile: *Kama wanawake ni wengi katika jamii, kama mwanamke ni tasa, kama mwanamke ni mjane pamoja na kama mwanamke hakutoshelezi,* majibu hayo yaliashiria kushindwa kuelewa matakwa ya swali. Kielelezo Na. 5.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi.


5 (i) Njia ya Uzazi wa mpango
(ii) Njia ya kutumia kalenda ya Uzazi
(iii) Njia ya Uke mwenza
(iv) Njia ya kutumia Vitamzi
(v) kufunga kizazi kwa mwanamke au
Mwanaume.


Kielelezo Na. 5.2: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 5

Katika kielelezo Na 5.2 mtahiniwa ametaja njia za uzazi wa mpango na ruhusa ya kuowa mke zaidi ya mmoja badala ya njia zitakazowezesha taasisi ya ndoa kufikia malengo yake kimalezi na kuimarisha maadili mema kwa watoto.

### 2.2.4 Swali la 6: Historia ya Uislamu Baada ya Kutawafu Mtume (S.A.W)

Swali hili lilitoka katika mada ndogo ya Ukuaji na Uendeshaji wa Dola ya Kiislamu wakati wa Makhalifa Wanne Waongofu. Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kufafanua sababu mbili za kuporomoka kwa Dola ya Kiislamu aliyoiacha Mtume (S.A.W). Swali hili lilipima umahiri wa watahiniwa kutathmini Historia ya Uislamu baada ya kutawafu Mtume (S.A.W) na kubaini sababu zilizosababisha kuanguka kwa Dola ya Kiislamu iliyoasisiwa na Mtume Muhammad (S.A.W).

Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa wote 84,230 (100%) walifanya swali hili. Kati yao watahiniwa 61,634 (73.17%) walipata alama 0 hadi 1.5 ambao ni ufaulu dhaifu. Watahiniwa 17,279 (22.89%) walipata alama 2 hadi 3.5 ambao ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 3,317 (3.94%) walipata alama 4 hadi 5 ambao ni ufaulu mzuri. Aidha, kati ya watahiniwa waliopata alama dhaifu, watahiniwa 43,834 (52.04%) walipata alama 0. Muhtasari wa ufaulu wa watahiniwa hao katika asilimia ni kama unavyoonekana katika Chati Na. 6.




**Chati Na 6:** *Asilimia ya ufaulu wa watahiniwa katika swali la 6*


Chati Na. 6 inaonesha ufaulu dhaifu wa watahiniwa katika swali kwa kuwa asilimia 73.17 walipata alama 0 hadi 1.5 ikilinganishwa na asilimia 26.83 ya waliofaulu. Hali hii imesababishwa na watahiniwa wengi kukosa maarifa kuhusu mada ya Historia.

Uchambuzi uliofanyika katika majibu ya watahiniwa umeonesha kuwa, watahiniwa waliopata alama hafifu hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Historia ya Uislamu baada ya Kutawafu Mtume (S.A.W) hadi hivi leo na wengine walishindwa kubaini matakwa ya swali hivyo walishindwa kujibu kwa usahihi swali hili.

Baadhi ya watahiniwa hao walitoa hoja kama vile; *Kutokuwepo kwa kiongozi bora mwenye kusimamia haki na amani. Pia, viongozi walikuwa hawana imani na viongozi wao, ambapo walisimamia wakiangalia khofu pamoja na madaraka kwa kuwa na majivuno ya kuongoza.* Mwingine aliandika; *Madai ya Makafiri juu ya dini baada ya kutawafu Mtume (S.A.W) pamoja na kulingania dini ya Uislamu.* Mwingine aliandika: *Kuporomoka kwa uchumi wa dola ya Kiislamu na vita vya Mayahudi pamoja na Mtume (S.A.W).* majibu haya yaliashiria kukosa maarifa ya kutosha katika mada iliyounda swali.


Mtahiniwa mwingine aliandika kuwa: *Kuacha kufanya ibada na kumshirikisha Allah (S.W) na imani thabiti.* Pia, wapo walioandika: *Viongozi kushindwa kufuata haki na usawa katika jamii pamoja na watu kutosimamisha dola ya Kiislamu kwa uaminifu kama nyakati za Mtume (S.A.W).* Wengine walijibu: *Kuvunjika kwa mkataba pamoja na*

*kuharibika kwa usahihi wa dini ya Kiislamu*. Pia wapo walioeleza:- *Maswahaba kutojua kuwa baada ya kufa kiongozi anatakiwa akae kiongozi mwengine katika uongozi pamoja na uongozi kutakiwa na wasiokuwa waislamu*. Vilevile, wengine walitaja:- *Kutoaminiana waislamu kwa waislamu pamoja na kumzulumu muislamu mwenzio juu ya mali yake.* Watahiniwa hao walionesha kutokuwa na maarifa kuhusu Ukuaji na Uendeshaji wa Dola ya Kiislamu wakati wa Makhalifa Wanne Waongofu. Kielelezo Na. 6.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.


6 (i) Kuvunjika kwa mkataba sababu ya kuporomoka kwa dola ya kiislamu aliyoacha mtume (s.a.w) kuvunjika kwa mkataba ndiyo chanzo ambacho cha kuporomoka kwa dola ya kiislamu.
(ii) Kuharibika kwa usahihi wa dini ya kiislam moja ya sababu ya kuporomoka kwa dola ya kiislamu aliyoiacha mtume (s.a.w) kuharibika kwa usahihi wa Quran ndani ya dini ya kiislamu.

Kielelezo Na. 6.1: Sampuli majibu yasiyo sahihi katika swali la 6

Pamoja na watahiniwa wengi kuwa na ufaulu hafifu katika swali hili, walikuwepo wachache ambao walionesha kuwa na maarifa kiasi kuhusu Ukuaji na Uendeshaji wa Dola ya Kiislamu wakati wa Makhalifa Wanne Waongofu. Watahiniwa hao walibaini matakwa ya swali hilo na kutumia maarifa yao kujibu. Aidha, majibu sahihi ya swali hilo yalikuwa: (i) *Mgogoro wa kisiasa uliozuka baina ya maswahaba wa Mtume (S.A.W) kuanzia kwa khalifa Othman bin Affan (R.A) mpaka kupelekea kuuliwa kwake*, (ii) *Njama za maadui wa Uislamu zilizopenyezwa kwa Waislamu kupitia kwa Myahudi Abdallah Bin Sabah ili kuchochea mfarakano uliopelekea kuanguka kwa dola aliyoiacha Mtume (S.A.W)* pamoja na (iii) *Mtihani wa Allah (S.W) kwa waumini hasa wale waliofuata baada ya Mtume (S.A.W) kwani Mtume (S.A.W) alitabiri hali hiyo na kutoa muongozo wa jambo la kufanya baada ya hali hiyo kujitokeza. Hivyo, Allah (S.W) ametimiza mtihani huo na kutoa uhuru wa maamuzi, aidha, kufuata njia ya kufaulu au kufeli.* Kielelezo Na. 6.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya sahihi ya mtahiniwa katika swali hili.



6 Kupitia fitina za makafiri za chi
ni kwa chini na kusababisha kuporomok
a kwa dola hiyo ya kiislamu aliyo lacha
mtume (saw). na kupeleka wai islamu
baadhi kuritadi kukatika dini zao zamwa
nzo.
Kugombaniana madaraka. wai islamu
waligombaniana madaraka wao wenyo
wo kwa wenyewe na kupeleke a
kupeleka waislamu ku achana na uislamu
na kuporomoka kwa dola ya kiislamu
nchini madinah.

Kielelezo Na. 6.2: Sampuli ya majibu sahihi ya swali la 6

### 2.2.5 Swali la 7: Nguzo za Uislamu

Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kubainisha sababu mbili za ulazima wa kumshuhudia Mtume (S.A.W) katika Shahada ya Pili. Swali lilipima umahiri wa watahiniwa kuchambua umuhimu wa kumshuhudia Mtume (S.A.W) katika kutamka Shahada ya Pili.

Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa wote 82,230 (100%) waliofanya mtihani walijibu swali hili. Kati yao watahiniwa 70,709 (83.95%) walipata 0 hadi 1.5 ambao ni ufaulu dhaifu. Watahiniwa 12,156 (14.43%) walipata alama 2 hadi 3.5 ambao ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 1,365 (1.62%) walipata alama 4 hadi 5 ambao ni ufaulu mzuri. Aidha, watahiniwa 67,226 (78.81%) kati ya watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu walipata alama 0. Chati Na. 7 inaonesha muhtasari wa ufaulu wa watahiniwa hao kwa asilimia.




**Chati Na. 7:** *Asilimia ya ufaulu wa watahiniwa katika swali la 7*


Chati Na. 7 inaonesha kuwa ufaulu wa jumla katika swali ulikuwa dhaifu kwa kuwa asilimia 83.95 walipata alama za chini, ikilinganishwa na asilimia 16.05 waliopata ufaulu mzuri. Uchambuzi uliofanyika katika majibu ya watahiniwa umebaini kuwa, watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana na umuhimu wa Shahada.

Baadhi ya watahiniwa hao walitoa tafsiri ya Shahada ya pili badala ya kueleza sababu zinazoonesha ulazima wa kumshuhudia Mtume (S.A.W) katika Shahada hiyo, watainiwa hawa waliandika; *Nashuhudia kuwa Mtume ni mjumbe wa Allah pamoja na nashuhudia kuwa Mtume ni Mtume wa mwisho* na wengine waliotoa tafsiri ya moja kwa moja, kama vile: *Mtume ni mjumbe wa Allah*, mwingine alijibu*: Ya kuwa unashuhudia kuwa Mtume Muhammad ndiye Mjumbe wa Allah na ndo kipenzi chake*. Majibu ya watahiniwa hawa yaliashiria kushindwa kuelewa matakwa ya swali.

Wengine walitafsiri shahada kama utakaso pamoja na dua ya kujikinga kwa Allah kutokana na shetani aliyelaaniwa (Al-istia'dha), kama vile; *Muislamu yeyeote anaetamka shahada huwa anamlaani shetani katika mwili wake na huwa anajiitakasa kiroho na kumtakasa Mtume Muhammad (S.A.W) na kutakasa kwa nafsi pamoja na sababu ya mtu kufaulu duniani na akhera. Muislamu anapotamka Shahada huwa anajitakasa kimwili na kiroho ni sababu ya mwanandamu kufaulu duniani na akhera*. Wengine walijibu; *Kumlaani sheitwani na kutakasika kwa roho pia ni sababu ya mtu kufaulu duniani na akhera*. Wengine walieleza:- *Kumtakia mema Mtume na kuwaombea Waislamu wote*. Wengine walijibu: *Ni lazima au amri ya Mwenyezi Mungu na*

*kutamka Shahada ya Pili ni kumlaani sheitwani*. Wengine walijibu:- *kwa sababu ya kutaka kumpwekesha Allah (S.W) na Kuwa na yaqini moyoni juu ya Kuumbwa kwake*.


Mwingine alieleza: *Shahada ni kiingilio cha mtu katika Uislamu na Shahada ni kumsifu Allah (S.W) kuwa hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki ispokuwa Allah (S.W)*. Mwingine alieleza: *Kutofanya hivyo au kutoamini kuwa Muhammad (S.A.W) ni Mtume wa Allah na kukufuru ni uasi na chanzo cha kuangamia duniani na akhera  na pia kumpa cheo kwa kumpa mamlaka ya kuongoza umma wa uislamu*. Mwingine alieleza: *Ili Shahada iweze kukamilika na kutofanya hivyo au kutoamini kuwa Muhammad (S.A.W) ni Mtume wa Allah (S.W) na kukufuru ni uasi na chanzo cha kuangamia duniani na akhera*. Majibu hayo ya watahiniwa yaliashiria kukosa maarifa ya kutosha kuhusu maana na umuhimu wa Shahada kama nguzo ya Uislamu. Kielelezo Na. 7.1 kinaonesha mfano wa majibu yasiyo sahihi ya mtahiniwa katika swali hili.


07 (i) Kumlaani sheitani na kutakasika kwa roho
Muislamu yeyote anaetamka shahada
kuwa anamlaani shetani katika mwili wake na
kuwa anajitakasa kiroho na kumpakasha Mtume
Muhammad (S.a.w) na kutakasika kwa roho;
na kuamini akuna mwingine apasae kuabudiwa ni
allah (S.w) pekee.
(ii) Sababu ya mtu kufaulu duniani na akhera:
Muislamu anapotamka shahada, huwa ana
jitakasa kimwili na kiroho ni sababu ya
Mwanadamu kufaulu duniani na akhera kwa
kuwa Unaamini Uwepo wa allah na Mtume
(S.a.w) pekee.

Kielelezo 7.1: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 7

Katika kielelezo Na. 7.1 mtahiniwa alitafsiri shahada kama njia ya kujitakasa na kuwa ni kinga kutokana na shetani aliyelaaniwa badala ya kubainisha sababu za ulazima wa kumshuhudia Mtume (S.A.W) katika Shahada ya pili.

Licha ya watahiniwa wengi (83.95%) kuwa na ufaulu dhaifu katika swali hili, walikuwepo watahiniwa wachache (16.05%) waliofaulu vizuri. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu Shahada na walielewa vema matakwa ya swali hivyo waliweza kubainisha hoja zinazoonesha ulazima wa kumshuhudia Mtume (S.A.W) miongoni mwa hoja hizo ni pamoja na: (i) *Mtume (S.A.W) ndiye aliyeteuliwa kufundisha juu ya uwepo, sifa na utukufu wa Mwenyezi Mungu (S.W) kwa kuwa yeye ndiye mpokezi wa ufunuo (Wahy) na* (ii) *Mtume (S.A.W) ndiye mfano unaobainisha namna sahihi ya kukamilisha lengo la kuumbwa kwetu (namna ya kumuabudu Mwenyezi Mungu). Hivyo, tunalazimika kumfuata Mtume (S.A.W) kwa kuwa yeye ndiye mfano wa jinsi ya kutekeleza ibada mbalimbali.* Kielelezo Na 7.2 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali la 7.


(7) Sababu za kumshuhudia Mtume (S.A.W) katika Shahada ya Pili ni:

(i) kumfata njia ~~ajafe~~ Ajate Muongozo kutoka kwa Mtume katika kuki endea kila kipengele cha Maisha yake.


(ii) Ili kumfanya mja Asimame katika Njia ya Haki Ambayo Mtume Alipewa na Allah(s.w)

Kielelezo Na. 7.2: Sampuli ya majibu sahihi ya swali la 7

### 2.2.6 Swali la 8: Mfumo wa Jamii ya Kiislamu

Swali hili lilikuwa na vipengele (a) na (b) kutoka katika mada ndogo ya Uchumi katika Uislamu. Katika kipengele (a) mtahiniwa alitakiwa kutofautisha mfumo wa uchumi wa Kiislamu na mifumo waliyobuni wanadamu katika dhana ya Umiliki wa mali. Katika kipengele (b) mtahiniwa alitakiwa kutofautisha mfumo wa uchumi wa Kiislamu na mifumo waliyobuni wanadamu katika dhana ya matumizi ya mali. Swali lilipima watahiniwa umahiri wa kuchambua dhana ya umiliki na matumizi ya mali kwa mtazamo wa Uislamu na Ukafiri.


Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa 84,230 (100%) walijibu swali hili, ambapo kati yao watahiniwa 58,356 (69.28%) walipata alama 0 hadi 1.5 ambao ni ufaulu dhaifu. Watahiniwa 15,889 (18.86%) walipata alama 2 hadi 3.5 ambao ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 9,987 (11.86%) walifaulu vizuri kwa kupata alama (4 hadi 5). Chati Na. 8 inaonesha muhtasari wa ufaulu wa watahiniwa hao kwa asilimia.




**Chati Na.8:** *Asilimia ya alama za watahiniwa katika swali la 8*

Chati Na. 8 inaonesha kuwa ufaulu kwa ujumla katika swali hili ulikuwa wa wastani kwa kuwa asilimia 30.72 ya watahiniwa walipata ala mzuri. Watahimiwa hao walionesha kuwa na maarifa kuhusu uchumi katika Uislamu hivyo waliweza kubainisha tofauti iliyopo baina ya mtazamo wa Uislamu na mtazamo wa Makafiri kuhusu dhana ya umiliki na matumizi ya mali.


Katika kipengele cha 8(a) watahiniwa hao walieleza tofauti iliyopo katika dhana ya umiliki wa mali kwa kuzingatia chanzo cha mali, kama vile: *Katika Uislamu mmiliki wa mali ni Mwenyezi Mungu (S.W) na umiliki wa mwanadamu ni dhamana hivyo atawajibishwa kwa jinsi alivyoichuma na kuitumia mali hiyo wakati katika mifumo mingine, umiliki wa mali ni ama wa kibinafsi au jumuiya na maamuzi yote juu ya mali hizo yanaisha kwa wamiliki.* Kielelezo Na. 8.1(a) kinaonesha mfano wa majibu sahihi ya mtahiniwa katika kipengele cha 8(a).



8 a) Dhana ya Umiliki wa Mali
Makafiri wanaamini kuwa mmiliki wa mali ni binaadamu ambaye ana uwezo kuitumia mali hiyo vyovyote vile anavyotaka Lakini Waislamu wanaamini kuwa mmiliki wa mali ni Allah (s.w) ambaye humruzuku mwanadamu kwa ruhusa yake mwenyewe.

Kielelezo 8.1(a): Sampuli ya majibu sahihi katika kipengele cha 8(a)

Aidha, katika kipengele cha 8 (b) watahiniwa hao waliweza kutofautisha dhana ya matumizi ya mali kwa kuzingatia mipaka ya matumizi iliyopo baina ya Uislamu na mifumo mingine kwa maelezo kuwa; *Sera ya Uislamu haitoi nafasi kwa mtu kufuja mali kwa vile anavyotaka pamoja na uhalali atakaokuwa nao katika umiliki wa mali hiyo wakati katika mifumo isiyokuwa ya Kiislamu mtu anayo fursa ya kufuja mali atakavyo maadamu yeye ndiye mmiliki wa mali hiyo.* Kielelezo Na. 8.1(b) kinaonesha mfano wa majibu sahihi ya mtahiniwa katika kipengele cha 8(b).



8 b) Dhana ya matumizi ya Mali
Makafiri wanaamini kuwa mwanadamu ana uwezo wa kutumia mali vile anavyotaka yeye bila ya kujali uhalali wala uharamu wake. Lakini Waislamu wanaamini kuwa Mwanadamu anatumia mali kwa kuchunga mipaka ya matumizi yake; katika halali na haramu


Kielelezo 8.1(b): Sampuli ya majibu sahihi katika kipengele cha 8(b)

Uchambuzi zaidi uliofanyika katika majibu ya watahiniwa umeonesha kuwa, watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi katika swali hili hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Uchumi katika Uislamu na wengine walishindwa kubaini matakwa ya swali.

Katika kipengele cha 8(a) baadhi ya watahiniwa hao walitoa maana ya umiliki wa mali badala ya kutofautisha dhana hiyo baina ya Uislamu na mifumo mingine. Watahiniwa hao waliandika: *Umiliki wa mali ni kitendo cha Mtu binafsi au ni kitendo cha kuhalalishwa mali.* Mwingine aliandika*: Dhana ya umiliki wa mali ni hali ya mtu kumiliki mali kama vile fedha, miradi au kitu chochote ambacho kinachoweza kumsaidia yeye katika maisha yake ya kila siku kwa kutumia mali alizokuwa nazo na ni za halali na siyo za haramu* na mwingine alieleza:- *Dhana ya umiliki wa mali ni kumiliki mali yako binafsi katika maisha ya kila siku mfano kama tajiri anavyomiliki mali yake.*

Wengine walieleza njia za kuchuma mali badala ya kutofautisha dhana ya umiliki wa mali, nao walieleza; *Kiislamu umiliki wa mali kwa chumo la Halali wakati Kikafiri umiliki mali kwa kuua au kufilisi,* na mwingine alijibu: *Uchumi wa Kiislamu hutumia Zakat na Sadaqat kutoka Msikitini lakini mfumo waliobuni watu hutumia kuuza na kununua mali.* Majibu hayo ya watahiniwa hayakuwa sahihi kwa mujibu wa swali husika jambo linaloashiria kuwa watahiniwa hao walishindwa kubaini matakwa ya swali katika kipengele hicho.

Aidha, watahiniwa wengine walitofautisha dhana ya umiliki wa mali kwa kueleza sifa ambazo hazikuwa sahihi katika mfumo mmoja au yote, kwa mfano; *Katika mfumo wa Kiislamu huwa mali ni ya Waislamu wote katika jamii wakati mfumo wa Kikafiri mali huwa ni ya mmoja mmoja.* Wengine waliandika; *Mfumo wa uchumi wa Kiislamu ni mfumo ambayo imeleta na Waislamu kwa ajili ya kuimarisha na kukuza uchumi wa Kiislamu mfano Benki za Kiislamu mali milki ya Waislamu wakati dhana ya umiliki mali ni hali ya mtu kumiliki mali yake binafsi mfano pesa shamba, nyumba n.k.* Wengine walieleza: *Dhana ya umiliki wa mali mfumo wa uchumi wa watu wanasema kwa katika umiliki wa mali wanatumia wanaume na wanawake hakuna kupewa mfumo wa Kiislamu ni sawa kwa sawa na Dhana ya utumiaji mfumo wa uchumi wa watu wanasema kwa katika utumiaji wa mali hakuna mwanamke kutumia mali bila ya kuruhusiwa na mwanaume.* Vile vile; *Dhana ya umiliki wa mali ni kuwasaidia watu wasiojiweza na wale hawana uwezo wa kuitafuta mali.* Majibu hayo ya watahiniwa yaliashiria kukosa maarifa ya kutosha juu ya mada ya Uchumi katika Uislamu. Kielelezo Na. 8.2(a) kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mtahiniwa katika kipengele cha 8(a).



8a Dhana ya umiliki wa mali
i Waislamu hutumia dhana hii kwa kutoa
zakka, sadaka au kuhiji. wakati.
Mifumo waliyobuni hutumika kustarekhe
pamoja na kuchafua jamii kwa zinaa.

Kielelezo 8.2(a): Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika kipengele cha 8(a)

Katika kielelezo Na. 8.2(a) mtahiniwa ameeleza dhana ya matumizi ya mali badala ya umiliki wa mali kwa mujibu wa Uislamu na mifumo mingine.


Kadhalika katika kipengele cha 8(b) watahiniwa wengi walionesha kukosa maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya matumizi ya mali na wengine kushindwa kubaini matakwa ya kipengele hiki. Baadhi ya watahiniwa hao walijibu kuwa; *Matumizi ya mali kwa mtazamo wa Uislamu ni ujenzi wa misikiti na kusaidia mayatima na wakati kwa mtazamo wa Kikafiri ni ujenzi wa baa na makumbi ya starehe.* Wengine walijibu:- *Mfumo wa Kiislamu hutumia mali kwa kuendeleza dola na kusaidia jamii wakati mfumo wa Kikafiri hutumika kama nyenzo ya kumdhoofisha asiye nacho na kumnyanyasa*. Majibu haya yalieleza mambo mahususi ya halali na haramu katika matumizi ya mali tofauti na matakwa ya swali ambalo mtahiniwa alipaswa kueleza kanuni ya jumla inayosimamia dhana ya matumizi kwa mujibu wa Uislamu na mifumo isiyokuwa ya Uislamu.

Wengine walichanganya baina ya dhana ya umiliki na matumizi badala ya kutofautisha dhana ya matumizi, watahiniwa hao waliandika: *Dhana ya matumizi ya mali ni Waislamu hutumia dhana hii kwa kutoa zakka, sadaka au kuhiji wakati mifumo waliyobuni hutumiaka kustarekhe pamoja na kuchafua jamii kwa zinaa.* Mwingine alieleza: *Dhana ya matumizi ya mali waislamu hutumia mali zao kwa kusaidia mayatima na wajane na mifumo waliyobuni hutumia mali zao kwa kutoa bidhaa na kutumia mali ya jamii.*

Aidha, watahiniwa wengine waliotoa maana ya matumizi ya mali, ambapo walieleza kuwa ni: *Dhana ya matumizi ya mali ni hali ambayo mali hiyo itatumika katika jamii ya watu ambao ni waislamu katika*

*mifumo mizuri ya kuendelea kiuchumi katika Uislamu mfano kuwasaidia masikini, kuendeleza misikiti katika jamii na kuwapa mafukara.* Wengine wakaandika; *Dhana ya matumizi ya mali ni ile hali ya kutumia mali yako au ulivyopewa kama Zakka au Swadakat.* Majibu haya yalionesha kuwa watahiniwa hao walishindwa kubaini matakwa ya swali katika kipengele hiki.

Baadhi ya watahiniwa walibuni hoja mbalimbali ambazo hazikuwa sahihi kwa swali husika, miongoni mwa hoja hizo waliandika; *Dhana ya Matumizi kwa mtazamo wa Kiislamu kipindi hicho waumini walikuwa wanatumia mali kwa kutoa Zakat na Sadaqat wakati hivi sasa mali hutumiwa katika kuendeleza mambo mbalimbali ya kijamii mfano ujenzi wa miundombinu, mambo ya kisasa n.k..* Wengine waliandika; *Dhana ya matumizi ni kuitumia mali kwa sheria iliyo sahihi kwa kufuata sheria za Kiislamu.* Majibu ya watahiniwa hawa yaliashiria kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Uchumi katika Uislamu. Kielelezo Na. 8.2(b) kinaonesha sampuli ya majibu yuasiyo sahihi ya mtahiniwa katika kipengele cha 8(b).


8 Dhana ya matumizi-ya mali
Waislamu hutumia mali zao kwa kusaidia
mayatima na wajane. Wakati,
Mfumo waliyobuni hutumia mali zao
kwa kutoa bidhaa na kutumia mali ya
jamii.

Kielelezo 8.2(b): Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika ipengele cha 8(b)


Katika kielelezo Na. 8.2 (b) mtahiniwa alitaja baadhi ya matumizi mahususi ya mali ambayo yanapendekezwa na sheria ya Kiislamu ingawa hakueleza kanuni ya jumla inayosimamia matumizi ama maamuzi ya mtu kutumia mali kwa namna hiyo.

### 2.2.7 Swali la 9: Haki na Uadilifu katika Uislamu.

Swali hili lilitoka katika mada ndogo ya Msimamo wa Uislamu juu ya Utumwa katika kipengele cha haki za maadui katika vita (mateka wa vita). Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kubainisha sifa mbili zinazoonesha ubatili wa vita au vurugu za watu waovu katika zama hizi

ambao wanatumia kivuli cha dini ya Kiislamu kueneza vurugu ama vita katika jamii. Swali lilipima umahiri wa watahiniwa kutathmini vurugu zinazoendelea katika jamii mbalimbali duniani kwa kunasibishwa na dhana ya Jihaad katika Uislamu.

Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa wote 84,230 (100%) walifanya swali hili. Kati yao watahiniwa 72,652 (86.25%) walipata alama 0 hadi 1.5 ambao ni ufaulu dhaifu. Aidha, watahiniwa 9,325 (11.07%) walipata alama 2 hadi 3.5 ambao ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 2,253 (2.67%) walifaulu vizuri kwa kupata alama 4 hadi 5. Watahiniwa 65,559 (77.83%) kati ya waliopata ufaulu dhaifu walipata alama 0. Chati Na. 9 inaonesha muhtasari wa ufaulu wa watahiniwa hao kwa asilimia.





**Chati Na. 9:** *Asilimia ya alama za watahiniwa katika swali la 9*

Chati Na. 9 inaonesha kuwa ufaulu wa jumla katika swali hili ulikuwa dhaifu kwani asilimia 86.25 ya watahiniwa katika swali walipata alama za chini. Watahiniwa hao walionesha kukosa maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya vita halali katika Uislamu na wengine walishindwa kuelewa matakwa ya swali husika. Aidha, uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unathibitisha maoni hayo kama ifuatavyo:

Baadhi ya watahiniwa hao waliandika madhara ya vita, kama vile; *Kuujumu uchumi na kujimilikisha wa mali,* wengine walieleza mafunzo ya vita mbalimbali kama vile Uhud na Badr na kuandika; *Chokochoko za Makafiri dhidi ya Waislamu hazitakwisha na pia ushindi wa Waislamu katika vita unatoka kwa Allah na si ubora wa silaha na wingi wa askari*. Wengine walieleza madhara ya kijamii kama vile: *Jamii*

*kugombana na kuchukiana wenyewe kwa wenyewe pamoja na kuanzishwa kwa misimamo migumu miongoni mwa wanajamii*. Hoja hizi hazikuwa sahihi kwa kuwa hazikuelekea kujibu hoja ya swali hivyo kwenda kinyume na matakwa ya swali husika.

Kundi lingine la watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki lilionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu vgezo vya vita halali kwa mujibu wa Uislamu, watahiniwa hao waliandika; *Watu waovu wanatumia kivuli cha dini ya Kiislamu kueneza vurugu na vita katika jamii wakificha malengo yao kiuchumi na kwa upande wa mavazi ya wanawake wa Kiislamu sasa yanatumika kama kinga ya watu kufanya maovu mpaka wakina baba wanatumia mavazi ya wanawake kama kinga kwao shungi (Nikabu)*, mwingine alijibu: *Kuwa mkweli na muwazi na kutetea jina la Mungu wako pale linapokosewa.* Wengine walieleza: *Dini ya Kiislamu ni ya amani na upendo na pia dini ya Kiislamu inaiasa jamii kudumisha amani na utulivu.* Mwingine alijibu*: Hakitosimama kiama hadi watu wapigane na wafanye vurugu zisizo za maana.* Majibu hayo ya watahiniwa yaliashiria kukosa maarifa ya kutosha juu ya mada husika. Kielelezo Na. 9.1 kimeonesha mfano wa majibu yasiyo sahihi ya mtahiniwa katika swali hili.



9) i) Jamii kugombana na kuchukiana wenyewe kwa wenyewe, kama vile kutofautiana katika mitimamo (madhehebu).
ii) Kuanjithwa kwa misimamo migumu miongoni mwa wanajamii, ambayo inapelekea vurugu.

Kielelezo 9.1: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 9

Katika kielelezo Na. 9.1 mtahiniwa alibainisha madhara ya vurugu hizo badala ya kutoa hoja zinazobatilisha ubatili wa vita ama vurugu hizo.

Pamoja na watahiniwa wengi (86.25%) kuwa na ufaulu dhaifu katika swali hili, walikuwepo pia watahiniwa wachache (13.75%) waliofanya vizuri. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu nidhamu za vita katika Uislamu na walibaini matakwa ya swali. Miongoni mwa hoja walizotoa ni pamoja na: (i) *Hawapigani ili kuondosha udhalimu katika jamii bali vita (fujo) nyingi zinapiganwa (zinafanyika ) kueneza udhalimu kwa kuwa makundi hayo yanayopigana*

*yanatumika kudhulumu haki za watoto, akina mama na wazee ambao hawana hatia yoyote . Mfano fujo zinazoendelea kaskazini mwa nchi ya Msumbiji,* (ii) *Hawapigani kuondoa uvamizi katika nchi bali makundi mengi yaliyoanzishwa na kunasibishwa na Uislamu yanavamia nchi zingine bila ya haki na kudai umiliki wa maeneo hayo,* (iii) *Vita halali haipaswi kuwa iliyosababishwa na uchokozi na namna yoyote, iliyosababishwa na kutukuza utaifa, iliyosababishwa na kujitanua kimipaka pamoja na iliyosababishwa kutafuta mateka, mali na mfano wake.* Kielelezo Na. 9.2 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali hili.


9. Sifa mbili zinazoonesha ubatili wa vita au vurugu hizo kwa mujibu wa mafundisho sahihi ya Uislamu.
i.) Dini ya Uislamu ni dini ya haki na usalama, kwani watu wote wanajisalimisha kwa Allah hivyo vurugu ambazo sio kwa ajili ya Allah hazikubaliwi katika dini ya Uislamu.

ii.) Dini ya Uislamu imepiga vita dhulma na kutoa roho kwani mwenye haki hiyo ni Allah (S.W) pekee yake, hakika jambo la umwagaji wa damu na vita havitakiwi katika uislamu kama inavyoelezwa katika Qur-an ( 2:30-32 ).

Kielelezo Na. 9.2: Sampuli ya majibu sahihi ya swali la 9


## 2.3 SEHEMU C: Maswali ya Insha

Sehemu hii ilikuwa na maswali manne ya insha kutoka katika mada za *Nguzo za Uislamu, Sunnah na Hadith, Qur'an na Dola ya Kiislamu Madina.* Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali matatu kati ya hayo. Kila swali lilikuwa na alama 15 hivyo sehemu hii ilikuwa na jumla ya alama 45.

### 2.3.1 Swali la 10: Nguzo za Uislamu

Swali lilitoka katika mada ndogo ya Kusimamisha Sala, ambapo mtahiniwa alitakiwa kueleza sababu tano za Waislamu kulazimika kusimamisha Sala tano kila siku katika maisha yao yote hapa duniani. Swali lilipima umahiri wa watahiniwa kuchambua ulazima wa kusimamisha Sala kama ilivyobainishwa katika Qur'an.

Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa 83,131 (98.69%) kati ya 84,230 (100%) walifanya swali hili. Kati yao, watahiniwa 29,278 (35.22%) walipata alama 0 hadi 4.5 ambao ni ufaulu dhaifu. Watahiniwa 34,224 (41.17%) walipata alama 5 hadi 9.5 ambao ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 19,629 (23.61%) walipata alama 10 hadi 15 ambao ni ufaulu mzuri. Chati Na. 10 inaonesha muhtasari wa ufaulu wa watahiniwa hao kwa asilimia.




**Chati Na. 10:** *Asilimia ya ufaulu wa watahiniwa katika swali la 10*

Chati Na. 10 inaonesha kuwa ufaulu wa jumla katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani asilimia 64.78 ya watahiniwa walifaulu vizuri ikilinganishwa na asilimia 35.22 ya watahiniwa waliopata alama hafifu.

Uchambuzi uliofanyika katika majibu ya watahiniwa umeonesha kuwa, ufaulu mzuri wa watahiniwa hao ulichangiwa na maarifa waliyokuwa nayo sambamba na kubaini matakwa ya swali. Aidha, watahiniwa hao walibainisha sababu hizo kwa ufasaha na kushajihisha majibu yao kwa aya na Hadithi mbalimbali za Mtume (S.A.W). Miongoni mwa majibu waliyoeleza ni pamoja na; (i) *Kusimamisha Sala ni amri ya Mwenyezi Mungu (S.W) ambayo imebainishwa wazi katika Qur'an katika Sura na*

*Aya mbalimbali mfano (29:45), (4: 103), (14:31) na nyinginezo,* (ii) *Kusimamisha Sala ni Nguzo ya pili ya Uislamu,* (iii) *Kusimamisha Sala ni nguzo kubwa ya Dini,* (iv) *Kusimamisha Sala ni kitambulisho cha Muislamu,* (v) *Kusimamisha Sala ni sababu ya kufuzu hapa duniani na akhera,* (vi) *Sala ndio amali ya kwanza kuhesabiwa siku ya Hesabu,* (vii) *Sala ni ufunguo wa Peponi na* (viii) *Kutosimamisha Sala ni miongoni mwa sababu kubwa ya watu kupewa adhabu ya Motoni.* Kielelezo Na. 10.1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali hili.


10 Sala ni maombi baina ya mja na
mola wake. Kusimamisha sala ni namna
ya kuswali kwa kufuata masharti yake
na nguzo zake na kuwa na khushui ili
kuweza kufikia lengo lake. lengo la swala
ni kumlinda mja kutokana na maovu na
machafu. Waislamu kulazimika kusimamisha
Sala tano kila siku katika maisha yao
yote hapa duniani kutokana na sababu
zifuatazo :-
Kusimamisha sala ni kutii amri ya
Allah (S.W). Allah (S.W) ameamrisha
katika kitabu chake baada ya kusema
" Simamisheni swala na toeni Zakka".
Waislamu wote wanatakiwa wasimamishe
swala kwa kutii amri ya Allah lengo
tu ni kupata mafanikio kwasababu
mwenyewe kasema yeyote atakaemtii
Allah na Mtume wake basi atakuwa
amefaulu. Hivyo waislamu wote wanatakiwa
kusimamisha swala katika maisha yao ya
kila siku ili kuja kupata mafanikio mbele
ya Allah.
Kusimamisha sala ni nguzo ya pili
ya Uislam. Mtume (S.A.W) amesema
katika hadithi yake kuwa uislamu
umejengeko katika nguzo tano nazo ni
kutoa shahadda 2, kusimamisha sala, kutoa
zakka, kufunga mwezi wa Ramadhan na
kuhiji kwa kila mwenye uwezo. Hivyo
kusimamisha sala ni nguzo ya uislamu
Kwahiyo hakuwezi kusimamika uislamu

10 wa mtu pindipo nguzo moja haipo na hapo mtu atakuwa sio muislamu kamili. Hivyo waislamu wote duniani wanalazimika kuswali swala tano ili kuweza kukamilika kwa uislamu wa mtu.

Kusimamisha sala ni kitambulisho cha uislamu wa mtu. Katika maisha ya ulimwenguni kila dini inavitambulisho vyake na dini kuu ya Uislamu kitabulisho chake ni kusimamisha sala. Hivyo kutokana na kusimamisha sala tunaweza kumtambua muislamu yupi na kafiri yupi Na kama hadithi zinavyoeleza kuwa tofauti ya Muislamu na Kafiri kuwa ni sala. Hivyo sala ni kitambulisho cha uislamu wa mtu.

Kusimamisha sala ni ufunguo wa peponi. Mtume (S.W) amesema kuwa swala ni ufunguo wa kila kheir. Muislamu anaposwali ipasavyo Allah (S.W) humuandalia kheir na kheir ambazo ~~zina~~ zinazotoka kwa Allah pamoja na kumuandalia pepo. Hivyo waislamu wanatakiwa wasimamishe swala tano wote waweze kuingia katika pepo ya Allah (S.W).

Vilevile kusimamisha swala ni ni nguzo ya Dini. Mtume (S.A.W) amesema kuwa Swala ndio nguzo kuu ya dini basi atakaesimamisha swala ~~amesimue~~ atakuwa ameisimamisha dini yake na atakaeicha swala atakuwa




Kielelezo Na. 10.1: Sampuli ya majibu sahihi ya swali la 10

Uchambuzi zaidi uliofanyika katika majibu ya watahiniwa ulibaini kuwa, watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi na kupata ufaulu hafifu (35.22%), walikosa maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Kusimamisha Sala. Wengine walishindwa kubaini matakwa ya swali husika hivyo, walijibu kwa kubainisha mambo mbalimbali ambayo hayahusiani na msingi wa swali lenyewe.

Baadhi ya watahiniwa hao walitaja Nguzo za Imani badala ya kueleza sababu za Waislamu kulazimika kusimamisha Sala tano, watahiniwa waliandika: *Kutambua kuwa Mwenyezi Mungu yupo, kuamini Siku ya Mwisho, kuamini Vitabu vyake na Kuamini Malaika wake.* Wengine walieleza faida ya kusimamisha Sala za Jamaa kama vile: *Hujenga ushirikiano katika jamii, hujenga upendo na undugu, hujizuia mwanadamu na maovu, humuwezesha mwanadamu kuwa msafi na*

*hujenga utii kwa viongozi.* Vile vile walikuwepo walioeleza njia za kumjua Mwenyezi Mungu na sababu za mwanadamu kushindwaa kuishi bila ya dini kama vile: *Maumbile ya mwanadamu, Maana halisi ya dini, vipaji alivyotunukiwa mwanadamu na nafasi ya fitra.* Majibu ya watahiniwa hao yaliashiria kuwa walishindwa kubaini matakwa ya swali.

Wengine waliotoa hoja ambazo hazikuwa sahihi kuhusu sababu za Waislamu kulazimika kusimamisha Sala tano, watahiniwa hao waliandika; *Kumuabudu, kumuomba Mtume lehema zake, kwa ajili ya kutubu zambi zetu, kusamehewa mambo mabaya, ili kujenga kizazi kizuri chenye heshima na ili kuwa mkalimu.* Vilevile, wengine walijibu kuwa; *Kushushwa kwa Qur'an, Elimu na ujuzi alionao mwanadamu, Lengo la kuumbwa mwandamu pamoja na milango ya fahamu aliyonayo mwanadamu.* Hoja za watahiniwa hao hazikuwa sababu za Waislamu kulazimika kusimamisha Sala tano bali hoja zinazoeleza mambo mtambuka katika Uislamu. Watahiniwa hao walionesha kuwa walikosa maarifa kuhusu Kusimamisha Sala.

Kwa ujumla watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu katika swali hili walishindwa kujenga hoja sahihi kuhusu sababu za Waislamu kulazimika kusimamisha Sala tano kila siku katika maisha yao yote hapa duniani. Hivyo, baadhi yao walipata alama hafifu na wengine walipata sifuri (0). Kielelezo namba 10.2 kimeonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hilo.

10 Kusimamisha swala; Ni kutekeleza masharti
yote ya swala na kufanya ibada bila kuacha
swala hata moja kuanzia mwanzo wa swala.
hadi mwisho wa swala. Zifuatazo ni sababu tano
za waislamu kulazimika kufanya ibada tano
kila siku katika maisha yao yote hapa duniani.
Utokusimamisha swala ni utakaso wa
nafsi; katika suala la kusimamisha swala
ni utakaso wa nafsi pia muislamu atawezo
kufanya ibada kwa sababu swala ina mtaka
sa mja kufanya ibada
Swala za jamaa huwafunza waislamu uo
ngozi bora; Waislamu wakifanya swala za jamaa-
wanaweza kuwa na uongozi ulio bora katika
maisho yao yote hapa duniani na kuwa na.
uwezo mzuri wa kufanya ibada au kusima
misha swala kwa ujumla.
Usafi na unadhifu wa mwili; Muisl
amu anatakiwa awe msafi wa mwili na unadhi
fi katika mavazi yake yawe na twahara kwa
ujumla kuwa na uwezo wa kufanyia ibada na
sehemu ya kuswalia.
Swala za jamaa zina malipo makubw
a kuliko swala ya mtu mmoja; katika kusim
amisha swala tunaambiwa kuwa swala ya
jamaa kuwa ni swala zenye maana kubwa sana
katika maisha ya kuwa swala ya jamaa
ina faida kuliko swala ya mtu mmoja in
dhamani ya swala kwa Muislamu ni kubw
wa sana

10 Swala za jamaa ~~huwafunza waislamu~~ huima
risha Undugu, Urawa, mshikamano; Pia kusimami
sha swala ya jamaa inaweza kuwa na Undugu -
Urawa na mshikamano katika kutekeleza ibada
ya swala ya jamaa
Yote kwa yote; kusimamisha swala ni muhim
u sana katika kutekeleza ibada ya swala katika
maisha yote ya hapa duniani kuwa inamalipo-
makubwa sana.


Kielelezo Na. 10.2: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 10

Katika kielelezo Na. 10.2 mtahiniwa ameeleza faida za kusimamisha Sala za jamaa badala ya kueleza sababu zinazowalazimisha Waislamu kusimamisha Sala tano kila siku katika maisha yao yote hapa duniani.

### 2.3.2 Swali la 11: Sunnah na Hadith

Swali lilitoka katika mada ndogo ya Uandishi wa Hadithi za Mtume (S.A.W) ambapo mtahiniwa alitakiwa kueleza sababu nne zilizosababisha kuwa na uandishi duni wa *Hadithi* wakati wa Mtume (S.A.W). Swali lilipima umahiri wa watahiniwa kutathmini historia ya uandishi wa Hadithi za Mtume (S.A.W) wakati bado akiwa hai.

Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa 72,978 (86.64%) kati ya 84,230 (100%) walifanya swali hili. Kati yao, watahiniwa 38,063 (52.16%) walipata alama 0 hadi 4.5 ambao ni ufaulu dhaifu. Watahiniwa 18,278 (25.05%) walipata alama 5 hadi 9.5 ambao ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 16,637 walifaulu vizuri kwa kuwa walipata alama 10 hadi 15. Chati Na. 11 inaonesha muhtasari wa ufaulu wa watahiniwa hao kwa asilimia.





**Chati Na. 11:** *Asilimia ya ufaulu wa watahiniwa katika swali la 11*

Chati Na. 11 inaonesha kuwa, ufaulu wa jumla katika swali ulikuwa wa wastani kwa kuwa asilimia 47.84 walifaulu vizuri ikilinganishwa na asilimia 52.16 waliokuwa na ufaulu dhaifu.

Uchambuzi uliofanyika katika majibu ya watahiniwa waliopata ufaulu mzuri umebaini kuwa, watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu historia ya Uandishi wa Hadithi za Mtume (S.A.W). Vilevile, waliweza kubaini matakwa ya swali. Watahiniwa hao waliweza kueleza

sababu zilizosababisha uchache wa uandishi wa Hadithi wakati wa Mtume (S.A.W) zikiwemo; (i) *Kuwepo kwa Mtume mwenyewe kama rejea inayoishi,* (ii) *Katika kipindi hiki Maswahaba walijishughulisha zaidi na kuandika, kusoma na kuhifadhi Qur'an vifuani mwao* (iii) *Mwanzoni Mtume (S.A.W) aliwakataza Maswahaba wake kuandika Hadithi akihofia kuwa watachanganya na Qur'an na* (iv) *Katika kipindi hiki pia Masahaba walishughulishwa zaidi katika harakati za kuuhami Uislamu ambao ulikuwa umezugukwa na maadui wengi.* Kielelezo Na. 11.1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali hili.



11 Hadithi. Ni taarifa au masimulizi juu ya matukio yaliyokuwa awali au mambo ambayo mtume akiyatenda na kutekeleza, kwa kulikataza au kuliondosha. zipiatazo ni sababu zilizosababisha kuwana uandishi duni wa hadithi wa kati wa mtume.

Mtume mwenyewe alikuwepo; hivyo hapa kuwana haja sana ya kuandika hadithi kwa sababu mtume-mwenyewe alikuwepo hivyo walishinikishana na kumwendea mtume kwa kumuuliza masuala mbalimbali.

Mtume mwenyewe alikataza uandishi wa hadithi Mtume alikataza uandishi wa hadithi katika kipindi cha utawala au cha uhai wake kwa kuwa usitiza Maswahaba kuhifadhi hadithi akidhani watachanganya na Qur'an.

Maswahaba walijishughulisha na uhifadhi-wa hadithi na kutekeleza katika matendo ya kila siku kipindi cha mtume na maswahaba hapa kuwa na uandishi mkubwa kwa sababu walishughulisha sana kuhifadhi hadithi na kutekeleza katika matendo ya kila siku hii ndiyo sababu ya uduni

Walijishughulisha na ulinganiaji na kusimamisha Uislamu katika jamii hivyo uandishi wa hadithi ulikuwa duni kipindi cha mtume kwa sababu alijikita katika kulingania na kusimamisha Uislamu katika jamii

Hivyo basi, kipindi cha maswahaba pamoja na Mtume hapakuwana uandishi mkubwa wa-hadithi, kwa sababu alihimiza maswahaba wajishughulishe na uhifadhi wa hadithi na akihofia watachanganya hadithi na Qur-an.


Kielelezo Na. 11.1: Sampuli ya majibu sahihi ya swali la 11

Uchambuzi zaidi ulibaini kuwa, watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu walishindwa kujibu kwa usahihi kwa sababu ya kukosa maarifa ya kutosha na kushindwa kubaini matakwa ya swali. Baadhi ya watahiniwa hao walitoa hoja ambazo hazikuhusiana na historia ya uandishi wa Hadithi, kama vile; *Uhaba wa elimu kutoka kwa waandishi, kusahau kuhifadhi vifuani mwao, kutozingatia vizuri walivyofundishwa na Mtume wao na kutohifadhi vifuani mwao na pia kufa kwa Mtume (S.A.W) na baadhi ya Maswahaba zake.* Wengine walijibu; *Mtume hakujua kusoma wala kuandika, hakukuwa na sayansi na teknolojia, walitumia njia ya kuhifadhi moyoni na sababu makafiri wangeweza kubadilisha.* na wengine; *Kutojua kuandika kwa usahihi, waandishi waliokuwa wakiandika walikuwa ni wachache, kwa sababu hawayakuyatilia maanani yaani walikuwa na migogoro kati yao na pia hawakuaminiana.* Hoja hizi zilionesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu Historia ya Uandishi wa Hadithi

Wengine walieleza:- *Teknolojia duni (hafifu), mazingira, hali ngumu ya maisha na kutokuwepo kwa waandishi wa kutosha.* Wengine walijibu:- *Uwepo wa vita dhidi ya wapinzani wa dini, uwepo wa Wanafiki, walijitolea kuwapambania waislamu katika vita ile na pia hapakuwa na vifaa vya kutosha vya kuandikia.*Wapo walioeleza:-*Maswahaba kuchanganya Sunnah na Hadith, kutokujua maana ya Sunnah na Hadith, kuchanganya matini na Rawi na kutokutofautisha Hadith sahii na kusahau kwa Maswahaba* na wengine; *Kuwepo kwa waandishi wengi wa Hadith, kuwepo kwa wapinzani wengi wa Hadith, Kuwepo kwa uchambuzi wa Hadith sahihi na zisizo za kweli na baadhi ya waandishi wa Hadith walikuwa wakiandika Hadith zisizokuwa za kweli.* Pia, wapo waliojibu*: - Ukosefu wa Vitabu vya kuandikia, ukosefu wa elimu ya uwandishi, Maswahaba walijikita katika mafundisho ya Mtume na kuwepo kwa waandishi wa uongo.* Wengine walieleza:- *Mtume hakujua kusoma wala kuandika, Mtume hakusoma sayansi na teknolojia, walitumia njia ya kifasihi kichwani pamoja na hakuwa na elimu ya kidunia*.

Kwa ujumla, baada ya kuangazia majibu mbalimbali yaliyotolewa na watahiniwa waliopata ufaulu wa chini, uchambuzi ulibaini kuwa, watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Sunnah na Hadithi hususani Uandishi wa Hadithi za Mtume (S.A.W).

Kielelezo Na. 11.2 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mtahiniwa katika swali hili.


11. Sunnah ya Mtume (S.A.W); Ni sunnah ambayo anakupa Mtume (S.A.W) na ina muhimu mkubwa katika maisha ya mwanadamu. Zifuatazo ni sababu zilizosababisha kuwa na uandishi duni wa Hadithi wakati wa Mtume (S.A.W).

Mtume hakujua kusoma wala kuandika; Ni moja kati ya sababu zilizosababisha kuwa na uandishi duni wa Hadithi wakati wa Mtume (S.A.W) hakujua kusoma wala kuandika.

Mtume hakusoma sayansi na teknolojia; Ni moja kati ya sababu zilizosababisha kuwa na uandishi duni wa Hadithi wakati wa Mtume (S.A.W). Ni kutosoma sayansi na teknolojia.

Walitumia njia ya kifasihi kichwani; Ni moja kati ya sababu zilizosababisha kuwa na uandishi duni wa Hadithi wakati wa Mtume Muhammad (S.A.W) walitumia njia ya kuhifadhi kichwani.

Hakuwa na elimu ya kidunia; Ni moja kati ya sababu zilizosababisha kuwa na uandishi duni wa Hadithi wakati wa Mtume (S.A.W). Mtume hakuwa na elimu ya kidunia.

Hivyo basi; Ndiyo sababu zilizosababisha kuwa na uandishi duni wa Hadithi wakati wa Mtume wetu Muhammad (S.A.W).


Kielelezo Na. 11.2: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 11

Katika kielelezo Na. 11.2 mtahiniwa ameeleza baadhi ya hoja ambazo hazikuwa sahihi kwa ushahidi wa kihistoria na zingine zinataja wasifu wa Mtume (S.A.W) badala ya kueleza sababu za uandishi duni wa Hadithi katika kipindi cha uhai wa Mtume (S.A.W).

### 2.3.3 Swali la 12: Qur'an

Swali hili lilitoka katika mada ndogo ya Ithibati ya Qur'an ambapo mtahiniwa alitakiwa kutumia hoja tatu kueleza namna ambavyo ujumbe wa Qur'an utawafikia wasiokuwa Waarabu na wasiojua lugha hiyo. Swali hili lilipima umahiri wa watahiniwa kutumia njia mbalimbali ambazo zitawezesha ujumbe wa Qur'an kuwafikia watu wote.

Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa 73,258 (86.97%) kati ya 84,230 (100%) walifanya swali hili. Kati yao, watahiniwa 37,227 (50.82%) walipata alama 0 hadi 4.5 ambao ni ufaulu dhaifu. Watahiniwa 26,834 (36.63%) walipata alama 5.0 hadi 9.5 ambao ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 9,197 (12.55%) walipata alama 10 hadi 15 ambao ni ufaulu mzuri. Chati Na. 12 inaonesha muhtasari wa ufaulu wa watahiniwa hao kwa asilimia.




**Chati Na. 12**: *Alama za watahiniwa kwa asilimia katika swali la 12*

Chati Na. 12 inaonesha kuwa ufaulu wa jumla katika swali hili ulikuwa wa wastani kwa kuwa asilimia 49.18 ya watahiniwa hao walifaulu vizuri ikilinganishwa na asilimia 50.82 ya waliopata ufaulu wa chini.

Aidha, majibu ya watahiniwa waliofaulu yameonesha kuwa, watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu Qur'an hususani Lugha ya Qur'an na walielewa vema matakwa ya swali hilo. Watahiniwa hao walieleza vema namna ambavyo ujumbe wa Qur'an utafika kwa wasiokuwa Waarabu na wasiojua lugha hiyo kwa hoja kama vile; (i) *Kutafsiriwa na kuelezwa kwa maandishi,* (ii) *Kutafsiriwa na kuelezwa kwa simulizi,* (iii) *Kuiga mwenendo wa Qur'an kwa wale walioupokea*

*na* (iv) *Kupitia athari inayopatikana katika nyanja zote za maisha zilizoangaziwa na Qur'an.* Kielelezo Na. 12.1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali hili.

12. Qur-an: Ni maneno kutoka kwa Allah (s.w) ambayo yameandikwa kwa lugha ya kiarabu aliyoshushiwa Mtume Muhammad (s.a.w) kipindi cha Ramadhan na malaika Jibril ambayo yamebeba mfumo na mwenendo mzima wa maisha ya binadamu na yamebeba ujumbe. Qur-an inaelezea mfumo mzima wa maisha ya binadamu pia inaelezea mambo mema ya kufanya ili kumpwekesha Allah (s.w) na inaorodhesha mambo mabaya yote na kukataza ili kujenga uislam uliokuwa bora. Zifuatazo ni namna au njia ambazo zitatumika kufikisha Qur-an kwa watu wasiojua kiarabu.

Kwa kuwasomesha madrasa: Wasiojua maana Qur-an kwa kiarabu wanapaswa kupelekwa madrasa ili waweze kujua maana ya kilichoandikwa kwa lugha yao. Kwa walimu kubwa madrasa wanasaidia watu kujua tafsiri ya Qur-an kwa lugha yao na kujua kusoma Qur-an kwa lugha ya kiarabu. kwahiyo watu wote wasiojua kusoma na maana ya Qur-an wanapaswa wasomeshwe madrasa ili waweze kujua maana ya kilichoandikwa kwenye Qur-an na jinsi ya kusoma Qur-an.

Kwa kutafsiri kwa lugha zao maana na lengo lake: Wasiojua maana ya Qur-an wanatakiwa kutafsiriwa kwa lugha zao ili waweze kupata lengo lake. Hali hii inaweza kusaidia watu waweze kujua ujumbe, maana na lengo la Qur-an kupitia tafsiri za lugha zao.


Kwa kuwafundisha kwa vitendo zaidi kuliko nadharia: Wasiojua maana ya Qur-an na lengo lake wanatakiwa kufundishwa kwa vitendo zaidi ili kuweza kuelewa kwa haraka zaidi na kuweka kichwani kwa haraka zaidi kuliko nadharia ambayo inaweza kuwababaisha watu kuchukua muda mrefu kujua na kuelewa lengo lake.

Hitimisho: Qur-an inaelezea muongozo mzima wa maisha ya binadamu pia inasaidia watu kuwa wacha mungu pia imekataza yale ambayo yamekatazwa na Allah (s.w) na imehimiza mambo yale ambayo yameamrishwa na Allah (s.w) yatendeke na waja wake.

Kielelezo Na. 12.1: Sampuli ya majibu sahihi ya swali la 12

Kwa upande mwingine, wengi wa watahiniwa waliopata ufaulu wa chini hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu Qur'an na baadhi yao walishindwa kubaini matakwa ya swali. Miongoni mwao waliandika hoja kama vile; *Kuongea na Mwenyezi Mungu nyuma ya pazia, Ndoto za kweli na kuagiza Malaika kufikisha ujumbe.* Majibu hayo yaliashiria kuwa mtahiniwa alishindwa kubaini matakwa ya swali husika hivyo, badala ya kueleza namna ujumbe wa Qur'an utawafikia wasiokuwa Waarabu na wasiojua lugha hiyo akaeleza njia anazotumia Mwenyezi Mungu kuwasiliana na waja wake. Vivyo hivyo, watahiniwa wengine walitoa hoja kama vile; *Kufunga mwezi wa Ramadhani, kuhiji pamoja na kwa ajili ya kumcha Allah.* Majibu hayo yaliashiria kueleza Nguzo za Uislamu badala ya njia ambazo ujumbe wa Qur'an utawafikia wasiokuwa Waarabu na wasiojua lugha hiyo.

Watahiniwa wengine walioshindwa kujibu kwa usahihi waliandika dondoo mbalimbali ambazo hazikujibu swali, miongoni mwa dondoo hizo waliandika; *Qur'an imeteremshwa kwa lugha ya Kiarabu kwa sababu ilifika kwa mjumbe wetu Muhammad (S.A.W), Qur'an imeteremshwa kwa lugha ya kiarabu kwani kulikuwa na lugha nyingi za makabila na Qur'an inajitosheleza katika kueleza maamrisho na makatazo aliyoamrisha Allah (S.W).* Mwingine alieleza: *Qur'an inatoa mafundisho pamoja na Qur'an inatoa mafunzo mema*. Wengine walitoa ufafanuzi kuwa: *Mwenyezi Mungu alishusha kiarabu lakini alimpa Mtume (S.A.W) kuzitafasili Kiarabu katika Kiswahili, Mtume amepewa uwezo na Mwenyezi Mungu kila akiteremshiwa sura yeye Mtume anazitafasili kwa lugha ya Kiswahili na Mwenyezi Mungu aliteremshwa Qur'an kidogo kidogo na kuzitafasili kwa Lugha ya Kiswahili*. Wengine walitoa hoja kama: *Mafanikio ya Hadithi, Mafanikio ya Mitume na Tawhid*. Kwa ujumla majibu hayo yaliashiria kukosa maarifa katika mada ya Ithibati ya Qur'an, hivyo walishindwa kutoa hoja sahihi kwa mujibu wa swali. Kielelezo Na. 12.2 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mtahiniwa katika swali hili.



12. Qur-an ni kitabu kilichoteremshwa na mwenyezi mungu na lengo kuteremshiwa mtume muhamadi lengo la kueneza dini kwa watu.
Upatao ni namna ambavyo Qur-an itafikisha ujumbe wake kwa wasiokua waarabu na wasiojua lugha hiyo.
Kuongea na mwenyezimungu nyuma ya pazia; hii ni namna mojawapo ya Qur-an kufikisha ujumbe kwa wasiokua waarabu na wasiojua lugha hiyo ni pale ambapo m/mungu atatuagiza mtume kuja kufikisha ujume kwa watu.
Ndoto za kweli; hii ni namna ya Quran kufikisha ujumbe kwa wasiokua waarabu na wasiojua lugha hiyo ni pale ambapo unakua umelala na kuanza kuota ndoto ambayo ni ya kweli.
Kuwaagiza malaika kufikisha ujumbe; hii ni namna ambayo Qur-an inaweza kufikisha ujumbe kwa wasiokua waarabu na wasiojua lugha hiyo ni pale ambapo mwenyezi mungu (S.w) anapowaagiza malaika kuja kueneza dini kwa watu.
Hivyo basi, hii ndiyo namna ambayo Qur-an inaweza kupeleka ujumbe kwa wasiokua waarabu na wasiojua lugha hiyo.


Kielelezo Na. 12.1: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 12

Katika kielelezo Na. 12.1 mtahiniwa alishindwa kubaini matakwa ya swali ambapo ameeleza njia anazotumia Mwenyezi Mungu kuwasiliana na waja wake badala ya kubainisha njia ambazo ujumbe wa Qur'an utawafikia wasiokuwa Waarabu na wasiojua lugha hiyo.

### 2.3.4 Swali la 13: Dola ya Kiislamu Madina

Swali hili lilitoka katika mada ndogo ya Uanzishwaji wa Dola ya Kiislamu Madinah ambapo mtahiniwa alitakiwa kutoa hoja nne kuthibitisha namna mkataba wa Madinah ulivyoimarisha mahusiano na mshikamano baina ya Waislamu na kuweka misingi ya mahusiano mema kati ya Waislamu na watu wa imani nyingine. Swali hili lilipima umahiri wa watahiniwa kutathmini mafanikio ya Mkataba wa Madinah uliowekwa baina ya Waislamu na jamii ya wasiokuwa Waislamu walioishi Madinah.

Watahiniwa 23,307 (27.67%) kati ya 84,230 (100%) walifanya swali hili. Miongoni mwao, watahiniwa 17,099 (73.36%) walipata alama 0 hadi 4.5 ambao ni ufaulu dhaifu. Watahiniwa 5,352 (22.96%) walipata alama 5.0 hadi 9.5 ambao ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 856 (3.67%) walipata alama 10 hadi 15 ambao ni ufaulu mzuri. Chati Na. 13 inaonesha muhtasari wa ufaulu wa watahiniwa hao kwa asilimia.




**Chati Na. 13:** *Asilimia ya ufaulu wa watahiniwa katika swali la 13*

Chati Na. 13 inaonesha kuwa, ufaulu wa jumla katika swali hili ulikuwa dhaifu kwa kuwa asilimia 73.36 ya watahiniwa wote walipata alama za chini ikilinganishwa na asilimia 26.64 ya waliopata ufaulu mzuri.

Uchambuzi uliofanywa katika majibu ya watahiniwa waliopata ufaulu wa chini ulibaini kuwa, watahiniwa hao walishindwa kujibu swali kwa usahihi kwa sababu ya kukosa maarifa ya kutosha kuhusu Uanzishwaji wa Dola ya Kiislamu Madinah na wengine walishindwa kubaini matakwa ya swali.

Baadhi ya watahiniwa hao waliandika kuwa; *Waislamu kupata fursa ya kuutangaza Uislamu ndani ya Bara Arab nzima, kukomboka kutokana na ujahili na kufuata mfumo sahihi wa maisha, kupatikana kwa mazingira ya amani na usalama.* Wengine: *Waislamu kupata fursa ya kulingania Uislamu Makka, Waislamu kupata fursa ya kukaa Makka na Wakaazi wa Makka walipata fursa ya Kusilimu pamoja na Waislamu walipata fursa ya kujiendeleza kiuchumi*. Wengine walijibu:- *kushirikiana katika shughuli za biashara halali ili kukuza maendeleo, waweze kumuabudu Allah (S.W) kwa pamoja, Ni kuwapokea Waislamu watakapokwenda katika mji wa Madina na kujenga udugu kama wa mji mmoja ili kusimamisha Uislamu*. Watahiniwa hawa walichanganya baadhi ya hoja za faida ya mkataba wa Hudaybiya badala ya kuangazia mkataba wa Madinah.

Wengine walieleza baadhi ya vipengele vya Mkataba wa Hudaybiya kama vile:- *Makurayshi walisema yoyote atakaetoroka Makka kwenda Madina wasimpokee, Waislamu walipata fursa ya kubakia Makka na kulingania Uislamu jambo ambalo lilipelekea kusilimu na Makuraishi mbalimbali mfano Sahil Bin Amir na Waislamu walipata fursa ya kujidhatiti kijeshi*. Majibu hayo yaliashiria kuwa watahiniwa hao walishindwa kuelewa matakwa ya swali.

Wengine waliandika baadhi ya mambo aliyoyafanya Mtume (S.A.W) alivyofika Madinah kama vile:- *Uliweza kuimarisha mkataba kwa kutengeneza Dola ya Kiislamu, kuweka mkataba na wasio Waislamu na kujenga Msikiti madina.* Wengine walijibu:- *Mtume alijenga ummah wa Kiislamu, Mtume (S.A.W) kukubali kipengele kinachosema kuwa kusiwe na Ugomvi baina ya makafiri na Waislamu na Makafiri, kuwepo uhusiano mzuri baina ya kabila la Aus na Khazraj na kuwepo kwa Mkataba wa Amani baina ya makabila yaliyo pembezoni mwa Madina.* Majibu hayo yaliashiria kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu Mkataba wa Madinah na kushindwa kuelewa matakwa ya swali. Kielelezo Na. 13.1 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 13.

13 Mkataba ni mkataba wa Amani
uliofunga baina ya waislamu na makuraishi.
mkataba huo ulifungwa TH kiongozi wa
waislamu ni Mtume muhamad (SAW) na
upande wa makuraishi ni sahil bin Amri.
kwa kuendelea na mtaba huo ulivyoimarisha
mahusiano baina ya pande zote mbili kama
ifuatavyo ;- kwa kuangia na upande wa
makuraishi kama ifuatavyo ;-
Waislamu watakapokuja Umra wak
ae siku tatu tu. makuraishi wa makka
waliwazuiya waislamu kwenda kufanya Umra
vile vile waliwapa siku tatu tu ya kufanya ibada
ya umra Waislamu walienda na walipofika
siku ya tatu ~~ttd~~ wakapanga safari ya kurudi
madina.
Makuraishi walisema yoyote atakae
tororka makka kwenda madina wasimpokee.
makuraishi waliwambia waslamu hapana ruhusa
ya kurudi madina ~~m~~ endapo wataenda madina
watakapourudi makka hawampokei arudi huko
kuko madina. kwa kuendelea na upande
wa Waislamu kama ifuatavyo ;-
Waislamu walipata fursa ya kubakia
makka na kulingania uislamu jambo amba
lo lilipelekea kuslimu wa makuraishi mbali
mbali mfano sahil bin Amri ndiye aliyesi
limu mwanzo ambae huyu alikuwa ni kiw
wa makuraishi kupanga mipango ya mkata
ba na vile vile waislamu walimarika na
kuendelea kulingania uislamu madina.
Waislamu walipata fursa ya
kujidhatiti kijeshi mfano mekaka TH waisl
amu waliwashinda makuraishi katika ngom
e ya tamur na vile vile walijimarisha
kijeshi katika kupambana na makuraishi
kuitetea dini ya ALLAH (SW) isipokue kwa
kwa mikono mtovu.
Kwa huyo namna mkataba huo uli
vyoimarisha mahusiano baina ya pande zote
mbili katika mkataba huo.

Kielelezo Na. 13.1: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 13

Katika kielelezo Na. 13.1 mtahiniwa ameeleza baadhi ya vipengele vya mkataba wa Hudaybiyah na faida za mkataba huo badala ya kutoa hoja zinazothibitisha namna mkataba wa Madinah ulivyoimarisha mahusiano

na mshikamano baina ya Waislamu na kuweka misingi ya mahusiano mema kati ya Waislamu na watu wa imani nyingine.

Kwa upande wa watahiniwa waliopata ufaulu mzuri, uchambuzi ulibaini kuwa watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu Uanzishwaji wa Dola ya Kiislamu Madinah na walielewa vema matakwa ya swali. Aidha, waliweza kuthibitisha namna mkataba wa Madina ulivyoimarisha mahusiano na mshikamano baina ya Waislamu na kuweka misingi ya nahusiano mema kati ya Waislamu na watu wa imani nyingine.

Miongoni mwa hoja walizoeleza watahaniwa hao zilikuwa; *Mkataba kusisitiza dhana ya umoja wa Waislamu wote bila kujali tofauti zao za kabila, taifa, vyeo au hali za kiuchumi, Kubainishwa wazi nafasi ya Mtume (S.A.W) kuwa ndiye mwangalizi mkuu mwenye wajibu wa mambo yote yanayowahusu Waislamu, Mkataba umeonesha wazi Uislamu hautofautishi maisha kiitikadi na kivitu hivyo muda wote Waislamu wanapaswa kuchunga mienendo yao kwa kuwa maisha yote yapo chimi ya mwamvuli mmoja wa muongozo,* na kwa upande wa mahusiano baina ya Waislamu na watu wa Dini zingine kulikuwa na hoja kama vile; *Mkataba kutoa uhuru kamili wa ibada na maoni kwa watu wote, Mkataba kulinda haki ya uhai wa mtu na mali zake* pamoja na *Mkataba kupinga uovu na udhalimu wa aina zote.* Kielelezo Na. 13.2 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa.

13 Mkataba wa Madina ulilenga - kuimarisha mahusiano na mashikamano - baina ya waislamu na kuweka misingi ya mahusiano mema kati yao na watu wa - imani nyingine. Nitathibitisha hoja hii kwa kuonesha namna mkataba huo ulivyoimarisha mahusiano baina ya pande zote mbili kwa kutoa hoja mbili kwa kila upande na nitaanza na upande wa Waislamu na kumalizia upande wa Imani nyengine ni kama ifuatavyo:-

Waislamu baada ya mkataba - waliweza kupata uhuru wa kufanya Ibada zao kwa utulivu bila ya kuwa na hofu yoyote ile. Kabla ya mkataba waislamu walikuwa hawapati muda mzuri wa kufanya Ibada zao walikuwa wakibughudhiwa na upande wa pili na kushindwa kutekeleza Ibada zao - kwa ukamilifu.

Waislamu kabla ya mkataba walikuwa ni wenye kupata matatizo mbali mbali kutoka kwa upande wa Imani - nyengine. Lakini baada ya mkataba walikuwa ni wenye amani na utulivu kwa - kufanya mambo yao ya kuwaletea faida ambazo wao walikuwa wakizitaka. Kabla ya mkataba ambao ulilenga mashirikiano na mashikamano.

13 Watu wa Imani nyingine wali
Kuwa hawana uhuru wa kufanya Ibada-
zao ambazo wenyewe wamejiwekea kama-
ni Ibada maalum zitakazo wafanya wao
Kuwa katika hali nzuri ya maisha, lakini
baada ya kuweka mkataba na Waislamu
walipata uhuru wa kufanya Ibada zao -
ambazo zilikuwa ni tofauti na za Waisla-
mu na Kuwa katika mahitaji yao wana
yo yahitajo wenye na Kupelekea Kuima
riha ~~na~~ mashirikiano na mashikamo.
Pia watu wa Imani nyengine
Kabla ya mkataba walikuwa ni watu -
wenye kuleta fujo na vita kwa waislamu.
Lakini baada ya mkataba ambao uliowe-
kwa kwa lengo la kuimarisha na -
kudumisha mshikamano baina ya pande
zote mbili na hatimae mashirikiano na
mshikamano yalipatakana baada ya-
pande zote mbili kuekeana mkataba.
Kwa hivyo hizo ndio hoja
ambazo nimezielezea zinaonesha jinsi -
mkataba wa madina uliyolenga kui
marisha mahusiano na mshikamano bain
a ya Waislamu na kuweka misingo ya
mahusiano mema kati yao na watu wa
Imani ngengine.

Kielelezo Na. 13.2: Sampuli ya majibu sahihi ya swali la 13

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU KWA KILA MADA

Mtihani wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu mwaka 2022 ulikuwa na maswali kumi na tatu (13) yaliyotolewa katika mada kumi na nane (18). Swali la kwanza liliundwa na mada kumi na tatu (13) ambazo ni; *Mtazamo wa Uislamu Juu ya Elimu, Imani ya Kiislamu, Kumjua Mwenyezi Mungu, Mtazamo wa Uislamu Juu ya Dini, Nguzo za Uislamu, Mtazamo wa Uislamu Juu ya Ibada, Mambo ya Lazima Kufanyiwa Maiti wa Kiislamu, Fiqh, Sunnah na Hadithi, Qur'an, Dini Sahihi anayostahiki Mwanadamu, Historia katika Uislamu,* na *Bara Arab zama za Jahiliyyah,* ambapo ufaulu wa jumla katika mada hizo ulikuwa asilimia 46.39.

Tofauti na swali la kwanza ambalo liliundwa na mada mbalimbali, maswali mengine kumi na mbili (12) yaliundwa kila moja kwa mada mahususi. Aidha, swali la 2, 7 na 10 yalitoka kwenye mada ya Nguzo za Uislamu, swali la 3 na 12 yalitoka katika mada ya *Qur'an,* swali la 4 lilitoka katika mada ya *Nguzo za Imani*, swali la 5 lilitoka katika mada ya *Familia ya Kiislamu*, la 6 lilitoka kwenye mada ya *Historia ya Uislamu Baada ya Kutawafu Mtume (S.A.W),* swali la 8 lilitoka katika mada ya *Mfumo wa Jamii ya Kiislamu* na la 9 lilitoka katika mada ya *Haki na Uadilifu katika Uislamu* wakati swali la 11 lilitoka katika mada ya Sunnah na Hadithi na swali la 13 lilitoka katika mada ya Dola ya Kiislamu Madinah.

Kati ya mada zote zilizotahiniwa katika mtihani huu hapakuwa na mada iliyokuwa na ufaulu mzuri. Aidha, kulikuwa na ufaulu wa wastani katika mada tano ambazo ni; *Sunnah na Hadithi (47.84%), Qur'an (47.17%), Nguzo za Uislamu (45.39%), Familia ya Kiislamu (44.05%),* na *Mfumo wa Jamii ya Kiislamu (30.72%).* Ufaulu huo wa wastani katika mada zilizotajwa ulichangiwa na kiwango kidogo cha maarifa waliyokuwanayo watahiniwa, ambao pia uliathiri uwezo wao katika kubaini matakwa ya maswali. Hali hizo zilisababisha kuchanganya hoja sahihi na zisizo sahihi katika majibu waliyotoa na baadhi kushindwa kufafanua vema hoja sahihi walizotoa katika majibu yao.

Kwa upande mwingine mada nne zilikuwa na ufaulu dhaifu katika mtihani huu ambazo ni; *Historia ya Uislamu Baada ya Kutawafu Mtume (S.A.W) (26.83%), Dola ya Kiislamu Madinah (26.64%), Haki na Uadilifu Katika Uislamu (13.75%)* na *Nguzo za Imani (11.61%)*. Ufaulu dhaifu katika mada hizo ulisababishwa na hali ya watahiniwa kushindwa kujibu maswali

waliyoulizwa kwasababu ya kukosa maarifa ya kutosha katika mada husika. Vile vile, kushindwa kubaini matakwa ya maswali na hatimae kushindwa kujenga hoja sahihi katika kujibu maswali kutoka kwenye mada hizo.

Muhtasari wa ufaulu katika mada hizo umeoneshwa katika Kiambatisho cha pekee, ambapo rangi ya njano imetumika kubainisha mada zenye ufaulu wa wastani na rangi nyekundu imetumika kubainisha mada zilizo na ufaulu hafifu.

## 4.0 HITIMISHO

Kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika Mtihani wa Kidato cha Nne (CSEE) 2022 somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu kilikuwa cha wastani hii ni kwa sababu asilimia 49.06 ya watahiniwa walifaulu. Aidha, uchambuzi umeonesha changamoto mbalimbali ambazo zinapaswa kutatuliwa ili kuboresha zaidi kiwango cha ufaulu katika mitihani ijayo ambazo ni watahiniwa kukosa maarifa ya kutosha katika mada mbalimbali hususani mada za *Historia ya Uislamu Baada ya Kutawafu Mtume (S.A.W)*, *Dola ya Kiislamu Madinah*, *Haki na Uadilifu Katika Uislamu* na *Nguzo za Imani*.

Kadhalika, kushindwa kubaini matakwa ya maswali, kushindwa kujenga hoja na kuzifafanua ipasavyo (hususani katika maswali ya majibu mafupi) pia kuchanganya hoja sahihi na zisizo sahihi katika kujibu maswali.

Ili kuinua zaidi kiwango cha ufaulu kwa mada zote katika mitihani ijayo, jitihada za ziada zinahitajika katika mchakato wa ufundishaji, ujifunzaji na upimaji endelevu wa wanafunzi shuleni. Jitihada hizo zinapaswa kulenga kuwajengea wanafunzi maarifa ya kutosha juu ya mada za somo ili wawe na uwezo wa kuelewa matakwa ya maswali na kujenga hoja stahiki.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuweza kuinua kiwango cha ufaulu katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu, yafuatayo yanapendekezwa:

(a) Walimu wanapaswa kuzingatia matumizi ya vitabu vya kiada na mbinu shirikishi katika ufundishaji ili kufikia umahiri uliyokusudiwa katika kila mada.

(b) Walimu wanapaswa kuwapima wanafunzi kwa muundo wa maswali ya umahiri yanayozingatia nyanja za juu za ufahamu ili kuimarisha uwezo wa wanafunzi na kuendana na mabadiliko yaliyopo.

(c) Wanafunzi wanapaswa kuzingatia mbinu za kusoma kwa kuelewa ili kuwa na uwezo wa kujenga hoja sahihi na kuzifafanua ipasavyo.

(d) Walimu wazingatie muhtasari wa somo baada ya kuufanyia uchambuzi ili waweze kufundisha kwa kuzingatia uzito wa kila mada.

**Kiambatisho Cha Pekee**

## Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa Katika Mada

| Na. | Mada | Ufaulu wa Kila Swali | | Asilimia ya Watahiniwa walio na wastani wa 30 na zaidi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Namba ya Swali | Asilimia ya Ufaulu | | |
| 1 | Sunnah na Hadithi | 11 | 47.84 | 47.84 | Wastani |
| 2 | Qur'an | 3 | 45.15 | 47.17 | Wastani |
| | | 12 | 49.18 | | |
| 3 | Mtazamo wa Uislamu Juu ya Elimu, Imani ya Kiislamu, Kumjua Mwenyezi Mungu, Mtazamo wa Uislamu Juu ya Dini, Fiqh, Mtazamo wa Uislamu Juu ya Ibada, Mambo ya Lazima Kufanyiwa Maiti Muislamu, Qur'an, Sunna na Hadithi, Nguzo za Uislamu, Historia katika Uislamu, Bara Arab zama za Jahiliyyah. | 1 | 46.39 | 46.39 | Wastani |
| 4 | Nguzo za Uislamu | 2 | 55.33 | 45.39 | Wastani |
| | | 7 | 16.05 | | |
| | | 10 | 64.78 | | |
| 5 | Familia ya Kiislamu | 5 | 44.05 | 44.05 | Wastani |
| 6 | Mfumo wa Jamii ya Kiislamu | 8 | 30.72 | 30.72 | Wastani |
| 7 | Historia ya Uislamu Baada ya Kutawafu Mtume (S.A.W). | 6 | 26.83 | 26.83 | Dhaifu |
| 8 | Dola ya Kiislamu Madinah | 13 | 26.64 | 26.64 | Dhaifu |
| 9 | Haki na Uadilifu Katika Uislamu | 9 | 13.75 | 13.75 | Dhaifu |
| 10 | Nguzo za Imani | 4 | 11.61 | 11.61 | Dhaifu |
| **Wastani wa Jumla wa Ufaulu katika Mada** | | | | **34.04** | **Wastani** |